# Nipashe

Jumatatu Februari 19, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581591

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
Maoni@guardian.co.tz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


**UCHAGUZI ACT**
Cheo cha Zitto chavutia vigogo



UKURASA 2

**NMB** yaipiga jeki serikali kutekeleza hoja ya CAG

UKURASA 4

**BOMOABOMOA**
ujenzi holela kutikisa katika Jiji la Dodoma

UKURASA 15



**GUARDIOLA AKATAA KUMLAUMU HAALAND**

UKURASA 22

# Hivi ndivyo mikopo umiza inavyoumiza

**ALIYEKOPA** Mil. 3/- atakiwa kurejesha Mil. 70/-, BoT yaonya mikopo hiyo imehamia mtandaoni... *Endelea ukurasa 8*



Sanamu ya Mwalimu Julius Nyerere ikiwa wazi baada ya kuzinduliwa Makao Makuu ya Umoja wa Afrika (AU) jijini Addis Ababa, Ethiopia jana. **PICHA: MTANDAO**

## Rais Samia atoa ujumbe mzito akizindua sanamu ya Nyerere

UKURASA 2

UKURASA WA 14

## MUDATHIR YAHAYA AGEUKA SHUJAA MPYA WA YANGA

KWA siku za karibuni, kiungo mkabaji wa Yanga, Mudathir Yahaya, amekuwa mkombozi wa baadhi ya mechi zinazoonekana...



## Bei ya sukari bado iko juu, wafanyabiashara watiwa mbaroni

UKURASA 3

**MICHEZO** WAWA AIONYA SIMBA, BENCHIKHA AFUNGUKA UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Cheo cha Zitto chavutia vigogo ACT - Wazalendo

**Na Halfani Chusi**

JOTO la uchaguzi ndani ya Chama cha ACT - Wazalendo limeendelea kupanda. Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Tanzania Bara, Dorothy Semu na Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria, Mbarala Maharagande, wamechukua fomu kuwania nafasi ya Kiongozi Mkuu wa chama hicho, ambayo sasa iko chini ya Zitto Kabwe.

Akifungua pazia la kunadi sera zake, Dorothy, baada ya kuchukua fomu jana, alisema atahakikisha chama hicho kinabaki kuwa sauti kuu ya Watanzania zinapotokea changamoto mbalimbali.

Pia alisema atahakikisha chama hicho kinakuja na sera mbadala zinazotekelezeka na kujibu shida za Watanzania na kuwaunganisha wanachama wote kuwa kitu kimoja.

Alisema atasaidia kufanya viongozi wao kuwa bora na kufanya chama hicho kuwa mfano. Anataka kukifikisha chama hicho kwenye ushindi utakaoweka rekodi.

"Nimeamua, ninaamni kwenye uongozi wa pamoja, nimekitumikia chama hiki kwa miaka minane katika nafasi mbalimbali, wakati chama kilipopita kwenye misukosuko ya kidemokrasia na mpaka kikataka kufutwa, nilisimama tulishirikiana na kuhakikisha kinapata hati safi," alitamba.

Naye Maharagande alisema ataitumia nafasi hiyo katika maeneo mengi ikiwamo kusimamia malengo na madhumuni ya chama, misingi yake, falsafa na itikadi.

"Nitahakikisha kwa kushirikiana na viongozi wenzangu, kwa kutumia njia mbalimbali tunashinikiza utekelezaji makubaliano kati ya Marehemu Maalim Seif na Dk. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar yanatekelezeka kwa vitendo na kwa ratiba mahususi.

"Nitashughulikia masuala ya demokrasia, siasa na uchaguzi kwa ujumla wake na kuhakikisha tunaendeleza madai ya kuwa na muungano wa haki na usawa wenye maslahi kwa pande zote mbili," alisema Maharagande huku akishangiliwa na wafuasi waliokuwa wamefurika katika ofisi za makao makuu ya chama hicho, Magomeni, Dar es Salaam.

Juzi, mwanachama Isihaka Mchinjita alichukua fomu kuwania nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa ACT Wazalendo Taifa, huku akijinadi akishinda nafasi hiyo, atasaidia kujenga chama.

Baada ya kuchukua fomu hiyo, Mchikita alisema kilichomsukuma kuchukua fomu ni mapenzi ya dhati, anataka kupigania demokrasia pana yenye maslahi ndani ya nchi, kuimarisha ngome za chama na kuzifanya kuwa nyenzo muhimu ya kuunganisha Watanzania kupigania haki na ustawi wa taifa.

Alisema atasaidia kujenga misingi imara ya kitaasisi, kuimarisha sera na mwenendo wa chama ili kisimame kama kiongozi mwenye kusukuma na kushinikiza utekelezaji agenda zenye maslahi kwa wananchi.

"Sote tunafahamu chama chetu kimepita katika hatua kubwa ya ukuaji ndani ya muda mfupi. Hiki ndicho chama chenye umri mdogo kuliko vyote nchini.

"Nafasi yangu ya uenyekiti wa mkoa niliyochukua Lindi nilikikuta chama hakina hata tawi moja, mpaka leo nimekiwezesha kuwa na uongozi uliokamilika kuanzia ngazi ya tawi, kata na mkoa. Hii inanipa ujasiri wa kuona ninaweza kutumikia nafasi ninayoiomba," alitamba.

Mbali na Mchinjita, watiania wengine walioji-tokeza ni Husna Sungura anayegombea nafasi ya ujumbe wa Kamati Kuu kupitia Kanda ya Pwani na Halima Nabalang'anya anayegombea nafasi ya ujumbe wa Kamati Kuu kupitia Kanda ya Kusini.




Rais Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye mazungumzo na Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, jijini Addis Ababa, Ethiopia jana. **PICHA: IKULU**

# Rais Samia atoa ujumbe mzito akizindua sanamu ya Nyerere

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka Waafrika kutambua kuwa umoja na ustawi wao upo katika idadi na hakuna anayeweza kuwa na ustawi wa kudumu bila Afrika yenye ustawi.

Alitoa kauli hiyo jana wakati wa uzinduzi wa sanamu ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere katika makao makuu ya Umoja wa Afrika (AU), Addis Ababa, Ethiopia.

Rais Samia ambaye aliwasili jijini Addis Ababa jana usiku, atahudhuria mkutano wa 37 wa wakuu wa nchi za Afrika ambao pamoja na mambo mengine, unatarajiwa kujadili kuhusu amani na usalama wa nchi za Afrika.

Katika ukurasa wa Samia Suluhu Hassan Channel, aliandika, "katika mkutano huu (wakuu wa nchi), pamoja na mambo mengine tutajadili kuhusu amani na usalama wa nchi zetu, sera na majawabu kuhusu elimu na ujuzi, ikiwa ni maeneo yanayogusa maisha ya wakazi zaidi ya bilioni moja wa nchi wanachama."

Uzinduzi wa sanamu hiyo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa barani Afrika, akiwamo Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema, Rais wa Kenya, William Ruto, Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi na Rais mstaafu wa Tanzania wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete.

"Ni kweli kusema upekee wetu unalingana na kutegemeana kwetu. Na kwa hivyo, kukamilisha ukombozi wa kisiasa na mabadiliko ya kiuchumi ni muhimu ili maisha yetu ya baadaye yawe salama. Makubaliano ya biashara huria ya bara lazima yatekeleze jukumu muhimu ili kuhakikisha ustawi na utu wa watu wa Afrika.

"Ni matumaini yangu kuwa kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere itahamasisha vizazi vya sasa na vijavyo kuwasha mwenge wao wenyewe katika kutafuta matumaini, upendo na utu pale ambapo hakuna," alisema.

Rais Samia alisema sanamu hiyo itadhihirisha mchango wake katika ukombozi, umoja na amani ya Afrika na fahari ya Bara la Afrika katika urithi wake mkubwa.

Alishukuru Umoja wa Afrika na wote walioshiriki kuandaa sehemu ya kuwekwa sanamu hiyo kama kumbukumbu muhimu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Rais Samia alirejelea maneno ya Mwalimu Nyerere wakati anapandisha Mwenge wa Uhuru katika kilele cha Mlima Kilimanjaro, kuwa alisisitiza kuleta amani na matumaini ndani na nje ya mipaka ya nchi, matumaini pale watu walipokata tamaa na upendo palipo na chuki.

"Ni matumaini yangu kuwa kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere itahamasisha vizazi vya sasa na vijavyo kuwasha Mwenge ndani yao katika kuendeleza upendo, matumaini na utu," alisema.

Alisema kuwa Mwalimu Nyerere alikuwa na maono makubwa na alijitolea ili kuwa na Afrika huru na yenye amani na kwamba aliweka mbele maslahi ya bara hilo kuliko maslahi yake binafsi au ya nchi yake.

"Hii inajidhirisha hata katika wimbo wetu wa taifa, ambapo tunaomba kwanza ustawi wa mama Afrika kisha kwa Tanzania," alifafanua.

Rais Samia alisema hata baada ya kuondoka madarakani, kiongozi huyo aliendelea kuunga mkono juhudi za Afrika, ikiwa ni pamoja na kuleta amani na kubakia bila kuyumba.

Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika, Moussa Mahamat, alisema Mwalimu Nyerere alikuwa mmoja wa viongozi mashuhuri aliyelifanyia Bara la Afrika mambo makubwa, ikiwamo kushiriki uanzishwaji wa AU mwaka 1963.

Alisema sifa kuu ya Hayati Mwalimu Nyerere ni kusisitiza umuhimu wa Afrika kushikamana na kuwa wamoja, akisema "Bara letu ni moja na sisi sote ni Waafrika, umoja huu (AU) linaashiria dhamira ya kusonga mbele."

Kwa mujibu wa Mahamat, hata alipohutubia Bunge la Tanzania, Mwalimu alikuwa akiwasisitiza wabunge kuungana na wenzao wa nchi za Kusini mwa Afrika kupigania uhuru, akisisitiza kuwa mapambano yao na ushindi wao ni kwa faida ya wote.

Alisema chini ya uongozi wa Hayati Nyerere, Tanzania ilikuwa kimbilio la harakati za uongozi katika bara zima, jambo linaloonesha namna kiongozi huyo alikuwa na ushirikiano katika ukombozi wa bara hilo.

Rais wa Jamhuri ya Zambia, Hakainde Hichilema, alisema sanamu hiyo ni ukumbusho wa mambo mazuri aliyoyafanya kiongozi huyo ikiwamo kupigania kuinuka kwa uchumi wa ukanda.

HABARI KITAIFA

# Walia sera za serikali si rafiki kwa viziwi

**Na Mwandishi Wetu**

VIONGOZI wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) wamesema kuna upungufu mkubwa katika utengenezaji sera za serikali kwa jamii ya viziwi.

Kutokana na upungufu huo, jamii ya watu wenye ulemavu huo inapata wakati mgumu katika shughuli zao za kila siku ikiwa ni pamoja na kutokuwa na vitendea kazi vinavyokidhi mahitaji yao.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa mfumo wa uchangiaji ujenzi wa kituo cha rasilimali na mafunzo cha chama hicho mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini CHAVITA, Joseph Hizza, alisema kituo hicho kitasaidia kuondoa vikwazo vilivyopo vya watu kutomtambua kiziwi.

Kituo hicho kikubwa Afrika Mashariki kinatarajiwa kugharimu Dola Marekani bilioni 6.4 sawa na Sh. bilioni 17.5 za Tanzania.

Mweyekiti wa CHAVITA, Selina Mayemba alisema kituo hicho pamoja na mambo mengine, kitaboresha maisha ya jamii ya viziwi kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ambayo yataboresha maisha yao.

"Kupitia uzinduzi huu wa uchangiaji ujenzi, niiombe jamii kupitia taasisi za serikali, watu binafsi na taasisi za kimataifa ili kuchangia ujenzi wa kituo hicho ambacho kitakuwa chachu kubwa ya maendeleo kwa viziwi na taifa kwa ujumla.

"Mfumo huo wa uchangiaji ni rahisi na mwepesi kwa kila mmoja kuanzia kiwango cha Sh. 100, hivyo kuwezesha watu wenye vipato mbalimbali kuchangia," alisema Selina.

Akiwasilisha andiko la mfumo huo wa uchangiaji unavyofanya kazi, Aneth Didas kutoka Kampuni ya Kolorio Innovation ya Dar es Salaam ambao ni waandaaji mifumo mbalimbali ya kidigitali, alisema kwa njia ya 'simu janja' pamoja na simu za kawaida, wachangiaji watakamilisha uchangiaji kiasi chochote cha fedha kwa kupitia simu zao za mkononi.

"Mchangiaji ataingia kwenye website ya Chavita ambayo ni www.deafdevelopment.or.tz atafuata maelekezo na kukamilisha changizo kupitia mitandao yote ya simu ambayo Watanzania wote wanatumia," alisema Aneth.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliyemwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, akifungua kitambaa kuashiria uzinduzi wa Hospitali ya Saifee Tanzania jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa hospitali hiyo, Murtaza Mamawala, Mwakilishi wa Bohora Tanzania, Janab Amil Saheb Sheikh Tayyebali na Mkurugenzi wa Idara ya Upasuaji Moyo, Hussein Hasanali. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Sukari yauzwa bei juu, wafanyabiashara mbaroni

**Na Waandishi Wetu**

LICHA ya serikali kuendesha misako ya mara kwa mara mkoani Mwanza na kukamata wafanyabiashara wa sukari wanaouza bidhaa hiyo kinyume cha bei elekezi, bei imeendelea kupanda, bidhaa hiyo ikiuzwa kati ya Sh. 4,500 na 5,000 kwa kilo.

Waandishi wa habari hizi jana walipita katika maduka mbalimbali ya jijini Mwanza na kubaini sukari ilikuwa inauzwa kwa bei tofauti na bei elekezi ya serikali ambayo ni Sh. 2,800 hadi 3,000 kwa kilo katika mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Wakazi wa Mabatini akiwamo Ester Joseph ambaye ni mamalishe, walisema wananunua bidhaa hiyo kwa Sh. 4,500 kwa kilo na kutaja hali hiyo kusababisha kuacha kuuza chai na vitafunwa vinavyotumia sukari kutokana na wateja kutoridhia kupandisha bei.

"Sasa nimeamua kuuza karanga na maisha yamekuwa magumu kwani wakati mwingine kilo tatu za karanga ninauza kwa siku nne tofauti na nilivyokuwa ninafanya biashara ya chai. Ninaomba serikali itazame upya suala hili," alisema Ester.

Mfanyabiashara wa Kahawa na Tangawizi, Juma Kilangwa, mkazi wa Mabatini alisema kwa sasa wateja wake wamepungua kutokana na kupandisha bei ya kikombe cha tangawizi ambayo awali aliuza kwa Sh. 200, sasa anauza Sh.300 mpaka 350.

"Tumeamua kupandisha bei ya kikombe kimoja cha chai kilichouzwa kwa Sh. 200 hadi kufikia Sh. 300 hii ni kutokana na sisi kupata sukari kwa bei ghali, lakini tumepoteza wateja kwani hawako tayari kubadili bajeti yao ya kila siku," alisema.

Judithi Kiwayo, mamalishe katika eneo hilo, alisema, "kila siku sukari inapanda bei, unaweza leo ukainunua kwa Sh. 5,000 baada ya siku mbili ukirejea wamepandisha mpaka Sh. 6,000, wakiona watu hawaelewi kila duka unalokwenda wanasema sukari hamna, mkikubaliana na bei sukari inapatikana, hili kweli ni tatizo na linatuumiza sisi watu wa chini vipato vyetu vyenyewe ni vya kusuasua, inaumiza sana."

Mfanyabiashara wa jumla wa bidhaa hiyo, maarufu Kido, alisema mfuko wa sukari wa kilo 25 anauza kwa Sh. 105,000 kutokana na upatikanaji wake kuwa mgumu. Mhitaji anapaswa kuamka usiku kwenda kupanga mstari kwa msambazaji mkuu wa Kanda ya Ziwa na wakati mwingine siku inaisha bila kupata bidhaa hiyo.

Mfanyabiashara mwingine wa jumla aliyejitambulisha kwa jina moja la Emmanuel, alisema hawapendi kuuza kwa bei hiyo, lakini nao pia wanauziwa kwa bei kubwa, wakijumlisha na usafiri, wanalazimika kupandisha bei, ili kurejesha fedha zao na kupata faida.

"Kwa bei elekezi mfuko wa kilo 25 tulitakiwa kununua kwa gharama isiyozidi Sh. 72,000, lakini tunanunua Sh. 100,000 hadi 105,000.

"Sasa hapo mtu ukimlazimisha auze bei elekezi atawezaje? Kwa sasa wanatakiwa wadhibiti bei hizo kutoka juu na pia kurahisisha upatikanaji wake ili tukinunua kwa bei hiyo na sisi tuuze kwa bei elekezi," alisema John Patrick, mfanyabiashara katika Mtaa wa Nyambiti.

Hivi karibuni baada ya kubainika kuwa Msambazaji Mkuu wa Sukari Kanda ya Ziwa amepandisha bei kinyemela, Mkuu Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana alitembelea duka na stoo ya msambazaji huyo ambaye aliahidi kuuza kwa bei elekezi.

Hata hivyo, msambazaji huyo alisema kuwa kuuza sukari kwa bei elekezi ni kufanya alichokiita kutengeneza hasara.

Juzi, Meneja wa Ufuatiliaji na Tathmini kutoka Bodi ya Sukari, George Fabian kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi mkoani hapa walifanya msako na kukamata wafanyabiashara wanne. Kati yao, watatu ni wa rejareja na mmoja wa jumla kwa tuhuma za kuuza sukari kwa bei ya juu tofauti na bei elekezi.

"Tunaendelea kuchukua maelezo kwa kushirikiana na polisi na jalada la uchunguzi litafunguliwa na kisha kufikishwa mahakamani ili kujibu tuhuma hizo," alisema Fabian.

Licha ya hatua hiyo iliyofanyika katika maeneo ya mjini, uuzwaji sukari kwa bei ya juu unaendelea katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Mwanza.

**-Imeandaliwa na Neema Emmanuel, Zatifa Ramadhan, Thomas Wandiba na Vitus Audax**

**KUPOTEA KWA CERTIFICATE OF INCENTIVE**

**FRANK SAMWEL SAMIKE**

Anatangaza kupotelewa na **TIC CERTIFICATE OF INCENTIVE FOR CRAFTY DEES BREWING COMPANY LIMITED** chenye usajili wa **So.NO.0224266** kilichotolewa na Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa polisi: **PHQ/DAR/KIN/22582/2024.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No 2712 of 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late PASKAL ANDREA MLOWO of mihuji within Dodoma City**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by DOREEN GADIEL MMARI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 4 day of 3......................... 2024

Dated at Dodoma this 14 day of 2........................2024

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA 3029 YA MWAKA 2024**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**
**ROBERT ALFRED MLAY..............MAREHEMU**
**MARTHA .J. SANGAWE NA**
**ALLEN . S. MLAY.............WAOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamiaji wa mirathi kwa waombaji walioomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 23 Mwezi wa Februari, Mwaka 2024

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 16 Mwezi wa February, Mwaka 2024

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA



Wanataaluma wa Chuo Kikuu Mzumbe wakiwa katika maandamano ya kitaaluma wakati wa kuuaga mwili wa marehemu Balozi Dk. Diodorus Buberwa Kamala katika ibada ya misa takatifu iliyofanyika Parokia ya Mwenyeheri Isidori Bakanja, Boko - Dar es Salaam jana. Balozi Dk. Kamala alifariki dunia Februari 12, mwaka huu na anatarajiwa kuzikwa mkoani Kagera Februari 20. **PICHA: LULU**

# NMB yaipiga jeki serikali kutekeleza hoja ya CAG

**Na Mwandishi Wetu**

MACHI 2017, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alitoa Ripoti ya Ukaguzi Maalum wa Miundombinu na Samani za Shule za Msingi Tanzania, akibaini hali mbaya ya miundombinu na samani za shule zinazomilikiwa na serikali.

CAG, kipindi hicho Prof. Mussa Assad, alitoa hoja kwamba serikali iboreshe mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi nchini kwa kuboresha miundombinu na samani zilizokuwapo na kujenga miundombinu mpya.

Katika kuisaidia serikali kutekeleza hoja hiyo ya CAG, Benki ya NMB imetoa msaada wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 80 ukiwa ni madawati 250 na mabati 368 kwa shule tano za Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, mkoani Mara.

Shule zilizonufaika na msaada huo ni Shule za Msingi Minigo iliyopata madawati 100; Nyanduru iliyopata madawati 100; Gilango iliyopokea mabati 168; na Kiamwani illiyopokea mabati 100, mbao na misumari.

Vilevile, Shule ya Sekondari Profesa Philemon Sarungi imejengewa hosteli mbili na kupewa Sh. milioni 15.

Mbali na misaada hiyo, benki hiyo pia imefanya ukarabati wa madarasa saba katika Shule ya Msingi Minigo pamoja na kumalizia ujenzi wa darasa moja katika shule hiyo.

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano iliyofanyika jana katika Shule ya Msingi Minigo, Mkuu wa Wilaya ya Rorya, Juma Chikoka alishukuru Benki ya NMB kwa kusaidia uboreshaji miundombinu ya elimu katika Wilaya ya Rorya.

Chikoka alikiri kuwa wilaya hiyo inakabiliwa na changamoto kubwa ya uchakavu wa miundombinu ya elimu, jambo ambalo liliibuliwa na CAG katika maeneo mengi nchini mwaka 2017, yaani miaka saba iliyopita na amekuwa akilitolea taarifa katika ripoti zake za kila mwaka.

"Misaada mbalimbali ya elimu tunayopokea kutoka NMB imeweza kuzisaidia shule zetu tatu za sekondari katika Wilaya ya Rorya zimeingia katika kumi bora ya Mkoa wa Mara katika mitihani ya taifa ya kidato cha nne," alisema.

Mkuu wa Wilaya huyo pia aliomba Benki ya NMB kufikiria kuwa mdhamini wa Tuzo za Elimu katika Wilaya ya Rorya zenye lengo la kusaidia shule zifanye vizuri katika mitihani ya kitaifa.

Chikoka pia aliomba benki hiyo iwasaidie kutoa mikopo ya wavuvi ili waitumie katika ufugaji wa vizimba na mikopo kwa wakulima ili wahamie kwenye kilimo cha umwagiliaji.

Kaimu Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Ziwa, Hamadan Sillia, alisema benki yao itaendelea kusaidia jamii kwa kuwa kushiriki katika kutatua changamoto mbalimbali zinazokabili jamii wanazohudumia ni moja ya vipaumbele vya benki hiyo.

"Ni faraja kwa Benki ya NMB kuona tunashirikishwa katika masuala muhimu kama utatuzi wa changamoto zinazoikabili jamii yetu, hii inaonesha ni namna gani mnaitambua Benki ya NMB kama sehemu ya jamii zenu, ni heshima na tunashukuru sana," alisema Hamadan.

Vilevile, Kaimu Meneja wa Kanda ambaye pia ni Meneja wa Benki hiyo Tawi la Kenyata Rod jijini Mwanza, aliomba walimu wa watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya kuendelea kutumia huduma mbalimbali za Benki ya NMB ikiwamo ufunguaji Akaunti za NMB Pesa ambazo hufunguliwa kwa Sh. 1,000 tu.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Minigo, Mwalimu Joseph Onyango alisema Benki ya NMB imesaidia kuongeza maudhurio ya wanafunzi kutokana na uboreshaji madarasa na wanategemea pia ongezeko la ufaulu.

Jedwali la uhaba wa miundombinu ya shule za msingi.

| Miundombinu | Mahitaji | Yaliyopo | Upungufu |
|---|---|---|---|
| Madawati | 596,872 | 438,806 | 158,066 |
| Vyoo (w'funzi) | 100,630 | 44,100 | 56,530 |
| Nyumba (wal) | 45,557 | 9,873 | 35,684 |
| Viti na meza | 63,764 | 33,935 | 29,829 |
| Madarasa | 57,866 | 30,550 | 27,316 |
| Ofisi walimu | 4,997 | 2,731 | 2,266 |
| Vyoo walimu | 1,520 | 898 | 622 |
| **JUMLA** | **871,206** | **560,893** | **310,313** |

**CHANZO:** Ripoti ya CAG, Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa 2021/22 (Uk. 116).

# Mabadiliko ya tabianchi yatajwa chanzo mgogoro kwenye shoroba

**Na Jenifer Gilla**

MENEJA wa Ushirikishwaji Sekta Binafsi katika Mradi wa USAID Tuhifadhi Mazingira kutoka Shirika la RTI, Dk. Elikana Ngallaba, amesema mabadiliko ya tabianchi ni moja ya vichocheo vya migogoro kati ya wanyamapori na binadamu kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ukame na uhaba wa chakula.

Ili kuondoa migogoro hiyo, ameshauri serikali kwa kushirikiana na taasisi binafsi, wadau wa uhifadhi kuzisaidia jamii zinazoishi katika maeneo ya mapitio ya wanyamapori (shoroba) kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia miradi mbalimbali.

Dk. Ngallaba aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akitoa mafunzo kwa waandishi wa habari yalioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) kupitia mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili.

Alisema mabadiliko ya tabianchi yanasababisha ukame ambao hupelekea vyanzo vya maji kukauka na kuathiri uzalishwaji chakula, hali inayopelekea wanyamapori kuvamia makazi ya watu wakitafuta maji ya kunywa na mifugo huku binadamu nao wakiwinda wanyama kutafuta chakula.

"Kwa hiyo, wanapokutana binadamu na wanyamapori tunaona migogoro inaongezeka, wanyama kama simba wanavamia mifugo, lakini wafugaji nao wanaingia mpaka maeneo yaliyohifadhiwa wakitafuta maji na malisho," alisema.

Dk. Ngallaba alisema ushirikiano wa pamoja kati ya serikali na sekta binafsi utarahisisha mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha wananchi wanakuwa na uwezo wa kuzalisha katika maeneo yao na kuondoa migogoro.

Alisema kupitia mradi huo wanashirikiana na wadau wengine kuhakikisha wanayatenga maeneo yenye shoroba na shughuli za wananchi ziendelee pasipo kuingilia mifumo ya wanyamapori kwa ili kuepusha migogoro hiyo na kuwakwamisha na shughuli za uhifadhi.

Alisema pia wanawawezesha wanavijiji hao kupitia miradi mbalimbali kwa kuwapa mikopo na mafunzo kwa ajili ya kuendesha biashara na kuwapa elimu na mbinu mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ikiwamo kufunga maeneo ya malisho kwa muda ili yasaidie kipindi cha ukame.

Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini wa mradi huo, Doroth Nyoni, alisema ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika uhifadhi kupitia mradi huo wanawake 1,872 watapatiwa mafunzo ya uongozi na mpaka sasa wameshawafikia 700 kuanzia ngazi za vijiji.

Alisema pia wanafanya kampeni za kuwafundisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wanaoishi kwenye mapitio ya wanyama namna bora ya kuhifadhi maliasili zilizoko katika maeneo yao kwa kuwapa elimu wakishirikiana na serikali.

Mkuu wa Kitengo cha Sera na Usimamizi wa Maliasili wa mradi huo , Allen Mgaza, alisema mbali na mabadiliko ya tabianchi wanyamapori pia wanapitia changamoto ya uwindaji haramu kwa ajili ya biashara.

Alisema ili kukabiliana na biashara haramu ya wanyamapori wizara, taasisi zisizo za kiserikali, wadau wa uhifadhi na jamii kwa pamoja washirikiane ili kuitokomeza kwa sababu inafanyika kwa usiri mkubwa.

Mkurugenzi wa JET, John Chikomo, alisema wametoa mafunzo ya mabadiliko ya tabianchi kwa waandishi wa habari, ili kuwaongezea wigo wa kuhabarisha jamii na kupunguza changamoto hizo hasa katika maeneo yenye shoroba.

Alisema JET imekuwa inatoa mafunzo kwa waandishi wa habari tangu mwaka 1991 ilipoazishwa ambayo yamekuwa endelevu na kuwafikia wengi zaidi katika kuongeza uelewa wa mazingira.

Alisema kwa sasa JET inatekeleza mradi wa tuhifadhi maliasili unaofadhiliwa na Mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili kwa miaka mitano kwa kuangalia shoroba saba nchini.

Jumla ya waandishi wa habari 20 wamepatiwa mafunzo hayo kutoka Tanzania Bara na Zanzibar ambao wamejumuisha kutoka vyombo vya serikali na binafsi.

TANGAZO

Friends of Lake Tanganyika

VNV Advisory

# TAARIFA KWA UMMA YA MKUTANO WA WADAU

Shirika la Friends of Lake Tanganyika (FOLT) la nchini Tanzania kwa pamoja na Kampuni ya Value Network Ventures Advisory Services (VNV) ya nchini Singapore wanatekeleza Mradi wa Gold Standard for Global Goals Standard Project ujulikanao kama **"Building Climate Resilience through Agroforestry Practices in Tanzania" (MRADI WA KILIMO MSETO),** unaotekelezwa katika Halmashauri za Wilaya ya Uvinza na Kasulu, Mkoani Kigoma-Tanzania.

Mradi huu una lenga kuwawezesha wakulima wadogo wadogo wapatao elfu tano (5000) mkoani Kigoma, kutekeleza kilimo endelevu (Kilimo Mseto) kwenye ardhi zao, ambacho kitaboresha rutuba ya ardhi mashambani mwao na hivyo kuongeza uzalishaji wa mazao ya aina mbali mbali na kuongeza Bioanuai mashambani. Aidha, Mradi utawezesha uhakika wa chakula (lishe) na kipato endelevu kutokana na ajira mbali mbali ambazo zitatokana na mradi huu.

Mradi huu unakusudiwa kuandikishwa na Gold Standard for Global Goals Standard kudai kupunguza uzalishaji wa hewa ya kaboni. Kwa taarifa hii, FOLT na VNV wanayo furaha kukualika kwenye mkutano wa mashauriano ya wadau wa mradi ili kujadiliana na kupata Maoni yako kuhusu mradi huu.

## RATIBA YA MKUTANO

**TAREHE:** 21 Machi 2024
**MUDA:** Saa 4 Asubuhi – 10 Jioni
**UKUMBI:** Viwanja vya Shule ya Msingi Katumbi, Kata ya Buhingu, Wilaya ya Uvinza, Mkoani Kigoma.

***Tunatarajia ushiriki wako katika mkutano huu. Ikiwa huwezi kuhudhuria, tafadhali tuma Maoni, mashaka na mrejesho wako kwenye anwani ya Katibu Mtendaji hapa chini:-***

## FRIENDS OF LAKE TANGANYIKA

**Kijiji cha Katumbi, Eneo la Makumbusho,**
**Wilaya ya Uvinza**
**S.L.P 1266 Kigoma**
**Barua pepe:**
**Friendsoflaketanganyika@gmail.com**
**Simu: +255 762175775**
**or**

## VALUE NETWORK VENTURES ADVISORY SERVICES

**10 Anson Road, #29-07 International Plaza, Singapore- 079903**
**Phone: +91 80 42429916,**
**+91 80 42429933, +91 9845017165,**
**+91 9739836912**
**Emails: madhureema@vnvadvisory.net**
**priyanka.mhaisne@vnvadvisory.net**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Imani hizi za kishirikina zinalitia doa soka letu

**KAMATI** ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), katika kikao chake cha Februari 14, mwaka huu kilikaa na kupitia mwenendo na matukio mbalimbali na kufanya maamuzi yake.

Yapo maamuzi ya mchezaji wa Prisons, Zabona Mayombya kufutiwa adhabu yake ya kadi ya pili ya njano iliyozaa nyekundu katika mechi dhidi ya Yanga ambapo ilibainika kuwa mchezaji huyo alidondoshwa na Bakari Mwamnyeto na hakuanguka mwenyewe kama tafsiri ya mwamuzi.

Mchezaji Jeremiaha Juma wa Prisons akafungiwa michezo mitatu kwa kumkanyaga kwa makusudi Yao Kouassi wa Yanga, na kutozwa faini ya Sh. milioni moja, mwamuzi Joseph Pombe wa Shinyanga kuondolewa kwenye ratiba ya waamuzi kwa kushindwa kutafsiri sheria, ambapo kwa ripoti kutoka kwa wakufunzi na watathmini wa waamuzi, alikataa bao halali la Kagera Sugar dhidi ya Yanga mechi iliyochezwa Uwanja wa Kaitaba, Februari 2, mwaka huu ikaisha kwa suluhu.

Matukio ni mengi, lakini kilichonishangaza ni matukio mengi yaliyoashiria imani za kishirikina, kumbe pamoja na maendeleo yote yanayopigwa na kuhubiriwa kwenye nyanja za michezo, bado kuna watu wanaamini ushirikina ili kupata ushindi.

Bado karne hii ya 21, wapo watu, viongozi na wachezaji ambao hawaamini kuwa na wachezaji wazuri, kocha bora, mazoezi, chakula, kambi bora, posho, mishahara mizuri, kupambana na kujituma ndiko kunakoleta ushindi, badala yake wameendelea kuamini mambo ya 'Kalumanzira' kuwa ndiyo yanayoleta ushindi.

Yanga kupigwa faini ya Sh. milioni moja kwa kosa la mashabiki wake watatu kuonekana kwenye eneo la vyumba vya kuvalia katika mechi dhidi ya Prisons, wachezaji wa timu hiyo ya Magereza, kutozwa faini ya Sh. milioni moja kwa kosa la wachezaji wake wa akiba kupitia dirishani badala ya mlango wakielekea katika mechi, hiyo yote inaonyesha ni dalili za imani za kishirikina.

Simba ikalimwa kiasi kama hicho kwa shabiki wake kuonekana akimwaga vitu vyenye asili ya unga kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, huwezi kulitenganisha na imani hizo.

Wachezaji wa Yanga, Kibwana Shomari kutozwa kiasi hicho kwa kuonekana akiondoa taulo la golikipa wa Mashujaa aliloliweka pembeni na wenzake Clement Mzize alifanya hivyo hivyo katika mechi dhidi ya Dodoma Jiji.

Hii ni kwa uchache tu, mengi hayajaorodheshwa na safari hii kumekuwa na adhabu nyingi sana za imani za kishirikina, kuliko wakati mwingine.

Tunadhani ifike wakati Shirikisho la Soka nchini (TFF), kupitia Bodi ya Ligi ikae chini kutafakari kupunguza kama siyo kukomesha kabisa matukio haya.


Yasiachwe tu kwa sababu yanaiingizia TFF na TPLB pesa, kinyume chake yanaishusha hadhi na kuonekana kama ligi fulani hivi ya mchangani, ambayo haina utaratibu na yeyote iwe kiongozi, mashabiki au mchezaji anaweza kufanya chochote na asifanywe lolote.

Ifike wakati timu zianze kukatwa pointi ili kukomesha tabia hizi, vinginevyo ile hadhi ya Ligi ya Tanzania kuwa moja ya ligi bora ambayo imetengenezwa kwa muda mrefu itashuka na kuonekana ya ovyo.

Nembo na heshima ya ligi ilindwe kwa gharama yoyote bila kuangalia pesa kwani kuendelea kuvumilia vitendo kama hivyo kunaichafua na kuishusha ligi yetu ambayo kwa sasa wachezaji wengi wakubwa wanavutiwa kuja kucheza nchini.

Hilo tumelioana na limethibitishwa kwa wachezaji wakigeni wanaocheza soka nchini kuitwa kwenda kuzitumikia timu zao kwenye michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon), kitu ambacho kwa miaka ya nyuma ilikuwa ni nadra sana kutokea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Usajili wa straika wa Mashujaa uwe somo kwa timu za Ligi Kuu

Na Adam Fungamwango

**HAKUTAJWA** wala kupewa nafasi sana kwenye uhamisho wa dirisha dogo la Ligi Kuu Tanzania Bara. Wapo wachezaji kutoka nje ya nchi hasa mastraika ambao usajili wao ulitikisa mno, lakini mpaka sasa wapo ambao wana bao moja na wengine hawana kabisa.

Viongozi wa Mashujaa FC nadhani wao wenyewe walijua nini wanafanya, wakaenda Stand United inayocheza Ligi ya Championship wakamsajili straika Emmanuel Mtumbuka.

Ulionekana ni wa kawaida sana, lakini mpaka sasa ndiyo usajili uliolipa zaidi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Straika huyo ana mabao mawili, akifunga katika mechi mbili mfululizo alizocheza mpaka sasa.

Mtumbuka ndiye mchezaji mwenye mabao mengi zaidi kati ya wote waliosajili kipindi cha dirisha dogo.

Akicheza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu katika historia ya maisha yake aliicheza dhidi ya Yanga, Februari 8, mwaka huu Uwanja wa Azam Complex, Chamazi akiingia kipindi cha pili, mpira wake wa kwanza tu alioupata akiwa mita 20, aliachia shuti kali lililojaa wavuni na kuisawazishia timu yake bao, kabla ya Yanga kuandika la pili baadaye.

> **Siku tatu baadaye, Februari 11, Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Mtumbuka, alifunga bao dakika ya 26 kwa mtindo ule ule wa shuti kali, lakini baadaye Dodoma Jiji ilisawazisha mechi ikaisha kwa sare ya bao 1-1.**

Siku tatu baadaye, Februari 11, Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Mtumbuka, alifunga bao dakika ya 26 kwa mtindo ule ule wa shuti kali, lakini baadaye Dodoma Jiji ilisawazisha mechi ikaisha kwa sare ya bao 1-1.

Wakati kuna wachezaji waliosajiliwa kwa pesa nyingi kutoka nje ya nchi wakiombewa kupewa muda wa kuzoea mazingira, yupo aliyetoka Championship anapiga mabao na anatikisa Ligi Kuu akitokea huko.

Sisemi kama klabu zisisajili wachezaji kutoka nje ya nchini, lakini kumezuka mtindo wa klabu za Ligi Kuu kusajili wachezaji ambao ni wale wale waliozoelewa na hawatupi kipya.

Mwaka wa 10, utakuta mchezaji anazunguka kutoka Mtibwa Sugar, kwenda Kagera Sugar, mara Dodoma Jiji, huyu huyo utamkuta msimu ujao KMC, halafu Namungo, mpaka inachosha.

Mtumbuka, anazikumbusha na kuzipa somo timu za Ligi Kuu, kuwa zianze kubadilika kuanzia msimu ujao.

Hata kama zitakwenda kusajili wachezaji nje ya nchi, lakini huku chini kuna wachezaji wenye vipaji ambao wanatakiwa nao kuingia taratibu katika ligi yetu kubwa. Ni kiasi cha kutenga muda wa kuwaangalia, kama Mashujaa walivyofanya kwa Mtumbuka.

Zamani wachezaji wengi wa Ligi Kuu walikuwa wanatoka kwenye madaraja ya chini, lakini kwa sasa wameonekana kama hawaaminiki.

Ni kweli viwango vya wachezaji wengi kwa sasa si kama vile, lakini wapo wenye uwezo wa kucheza Ligi Kuu vizuri tu kama upembuzi yakinifu ukifanyika, siyo kuchukuana kwa kujuana.

Ligi Kuu Tanzania imekuwa ikipokea wachezaji kutoka nje ya nchi, ni kitu kizuri, lakini imekuwa na uhaba wa kupokea wachezaji chipukizi wenye uwezo kutoka chini, kwa sababu wapo wachezaji ambao wanazunguka zunguka, huku uwezo wao ukiwa umefikia kikomo au hauwezi tena kupanda juu.

Hii si afya hata kwa kikosi cha Timu ya Taifa, Taifa Stars, tunahitaji kina Mtumbuka wengi kutoka Championship kwa ajili ya timu yetu ya Tanzania.

## HABARI KITAIFA

# CRDB, TCDC, TMX wapeleka kicheko kwa wakulima nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuendeleza jitihada za kuinua wakulima na wajasiriamali wa biashara ya mazao ya kilimo nchini, Taasisi ya CRDB Bank Toundation imetia saini mkataba wa ushirikiano na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Tume ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX).

Akizungumza kwenye hafla ya kutia saini mkataba huo, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Esther Mwambapa, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa mchango wa kilimo nchini ni mkubwa kuanzia kwenye uzalishaji chakula mpaka utoaji ajira hasa kwa wanawake na vijana, makundi yanayopewa kipaumbele na taasisi anayoiongoza.

"Azma ya taasisi yetu ya CRDB Bank Foundation ni kusaidia kuongeza ujumuishi wa kiuchumi, kuboresha maisha na kukuza ustawi wa jamii yetu.

"Ili kufikia malengo haya, CRDB Bank Foundation imekuwa ikibuni na kutekeleza programu mbalimbali za uwezeshaji kama vile programu ya IMBEJU ambayo hadi sasa imewafikia wanawake zaidi ya 125,000 na kutoa mitaji wezeshi zaidi ya Sh. bilioni tano," alisema Tully Esther.

Mkurugenzi huyo pia aliongeza kuwa CRDB Bank Foundation itashirikiana na mdau yeyote anayelenga kuwakomboa kiuchumi vijana na wanawake ilikuwapa nafasi ya kuujenga uchumi wa taifa.

"Ushirikiano huu unajielekeza zaidi kwenye sekta ya kilimo inayotoa ajira kwa zaidi ya asilimia 75 kwa watanzania na kuchangia asilimia 26 kwenye Pato la Taifa huku kikituhakikishia chakula kwa asilimia 95.

"Katika wilaya, tunatarajia kuzifikia walau Amcos (vyama vya ushirika) 10 ambazo tutaviwezesha kwa kati ya Sh. milioni moja mpaka Sh. milioni 30 au zaidi ya hapo kulingana na mahitaji yatakayokuwapo.

"Mkakati huu tunaamini utasaidia kukuza biashara ya wakulima na wajasiriamali wa kilimo," alisema Tully Easther.

Wakati CRDB Bank Foundation ikitarajiwa kutoa elimu ya fedha na ujasiriamali pamoja na mtaji wezeshi, TCDC itaratibu upatikanaji vyama hai vya ushirika huku WRRB ikihakikisha uhifadhi makini wa mazao ya kilimo na TMX ikiwakutanisha wakulima na wanunuzi wa mazao.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TMX, Godfrey Malekano alisema jukumu lao hasa ni kuhakikisha mkulima anapata bei nzuri ya mavuno yake. Tangu mwaka 2018, soko hilo lilipoanzishwa, alisema wameshayasajili mazao kadhaa ukiwamo ufuta, dengu, korosho, mbaazi na mazao ya mifugo na sasa hivi wanakamilisha utaratibu wa kuingiza madini.

"Soko linaendesha shughuli zake kwa kutumia teknolojia. Si lazima muuzaji na mnunuzi waonane. Kwa mkulima aliye mahali popote nchini, anaweza kuyaunza sokoni kwetu iwapo ameyapeleka kwenye ghala linalotambulika.

"Si lazima mnunuzi na muuzaji waonane, teknolojia inawaunganisha watu hawa. Ushindani unafanyika kwa uwazi wa hali ya juu na mkulima anapata bei nzuri zaidi sokoni," alisema Malekano.

Soko hilo pia, Malekano alisema linampunguzia mkulima gharama kwa kuwa anachotakiwa ni kuyapeleka mazao yake ghalani badala ya sokoni ambako si lazima amkute mnunuzi kwa wakati huo.

Akizungumza kwenye hafla hiyo iliyofanyika makao makuu ya Benki ya CRDB, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dk. Benson Ndiege alisema kuna zaidi ya vyama 7,000 vya ushirika nchini ambavyo sasa vitaanza kunufaika na mkakati uliowekwa na wadau wanaoenda kutekeleza.

Mtendaji Mkuu wa WRRB, Asangye Bangu, alisema huu ni mwendelezo wa kuwainua wakulima nchini. "Nguvu za kila mmoja wetu kwenye ushirikiano huu ni kubwa. Tunakwenda kuyatekeleza yote tuliyokubaliana hapa kumnufaisha mkulima wa Tanzania," alisema Bangu.



Kutoka kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Esther Mwambapa, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Asangye Bangu pamoja na Afisa Mtendaji Mkuu wa Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), Godfrey Malekano wakisaini mkataba wa ushirikiano wa kuwainua wakulima na wajasiriamali wadogo wa sekta ya kilimo katika hafla iliyofanyika mwisho mwa wiki iliyopita makao makuu ya Benki ya CRDB. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataka maboresho sera wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wenye Ualbino Tanzania (TAS) kimeomba serikali kuifanyia maboresho sera ya watu wenye ulemavu, hususani kundi la wenye ualbino, ili iendane na ongezeko la mahitaji ya kundi hilo na mabadiliko ya hali ya maisha kwa sasa.

Akizungumza katika mkutano wa watu wenye ualbino uliofadhiliwa na kampuni na taasisi mbalimbali ikiwamo Rotary Club Dar es Salaam, Rais wa TAS, Godson Mollel, mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam kuwa kutokana na ongezeko la watu wenye ualbino, mahitaji yao pia yameongezeka na kuna mabadiliko ya hali ya maisha na teknolojia ya kisasa katika utoaji huduma.

"Mazingira tuliyokuwa tunaishi jana hayafanani na leo, hivyo ni muhimu kufanyika maboresho ya mara kwa mara, ili huyu mwenye mahitaji maalum asiachwe nyuma. Kila serikali inapobadilisha sera ina uelekeo wa nchi, watufikirie na sisi wenye mahitaji maalum," alisema Mollel.

Rais huyo pia alitaka kuwapo kliniki inayotembea ili kurahisisha huduma kwa wanachama hao na kutokulazimika kwenda katika hospitali kubwa kupata mahitaji yao ikiwamo Taasisi ya Saratani Ocean Road ya jijini Dar es Salaam, Hospitali ya Rufani ya Kanda KCMC iliyoko Moshi auHospitali ya Rufani ya Kanda Bugando iliyoko jijini Mwanza kama ilivyo kwa sasa ambapo baadhi yao hulazimika kusafiri kutoka sehemu mbalimbali waliko na kwenda huko kupata huduma.

"Tunataka kliniki inayotembea, si lazima mwanachama wetu aende Ocean Road, si lazima aende KCMC, si lazima aende Bugando, huduma ya kliniki inayotembea ikiwapo maana yake ni kwamba wananchi watafuatwa mahali waliko," alisema Mollel.

Rais wa Rotary Club Dar es Salaam, Nazeer Tajudeen alisema waliamua kusaidia watu wenye ualbino kwa kuwa waliona ni wenye uhitaji zaidi kulinganisha na makundi mengine ya wenye ulemavu na kuhimiza jamii kusimama na kundi hilo.

"Kwa sasa tuna mpango wa kuandika vitabu kwa ajili ya watu wenye ulemavu, ili kujenga uelewa kwa jamii kuhusu mahitaji ya kundi hili na pia kuwafikia wadau mbalimbali, mashirika na taasisi mbalimbali ili watoe michango wao," alisema Tajudeen.

Alisema pia wanafuatilia kujua wanapoishi watu wenye ualbino na shughuli wanazofanya ili kuona ni namna gani wanaweza kuwasaidia katika kupata ajira na kujikwamu kiuchumi kupitia shughuli mbalimbali.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed






Mwendesha pikipiki akipita sehemu ya majitaka yatokayo katika chemba iliyopo eneo la Kamata jijini Dar es Salaam jana ikiwa ni tatizo la muda mrefu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# BoT yaonya mikopo umiza sasa imehamia mtandaoni

## - Aliyekopa mil. 3/- atakiwa kurejesha mil. 70/-

**Na Salome Kitomari**

MIKOPO umiza imeumiza watu! Kuna waliopoteza mali zao, kuhama mji na wengine kupoteza maisha kutokana na kutozwa riba kubwa, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imesema.

Kukiwa na hatari hiyo, BoT imeonya kuwa sasa kuna wimbi la wakopeshaji mtandaoni ambao masharti ya ukopaji yamegubikwa na usiri, hali ambayo ni maumivu kwa walaji.

BoT inatafsiri mtindo huo mpya wa ukopeshaji umejawa maumivu kwa wananchi, kwa kuwa mikopo umiza nayo imehamia mtandaoni.

Taasisi hiyo pia imesisitiza Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha imeweka masharti kila anayekopesha fedha, afuate taratibu na atakayekwenda kinyume adhabu ni faini ya Sh. milioni 10 au kifungo gerezani au vyote kwa pamoja.

Vilevile, BoT iko mbioni kutunga kanuni za uendeshaji biashara hiyo mtandaoni, lengo ni kuhakikisha Watanzania hawaumizwi na mikopo hiyo ambayo imechagizwa na ubunifu wa kiteknolojia.

Mwishoni mwa wiki, Ofisa Mkuu Mwandamizi Idara ya Huduma Ndogo za Fedha, Kurugenzi ya Usimamizi wa Fedha BoT, Deogratiaus Mnyamani, alielekeza hayo wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu sekta ya fedha nchini.

Alisema ni muhimu mwananchi anapopokea ujumbe kwenye simu ukimjulisha anaweza kukopa fedha, atafakari kwa kina, kutofuata maelekezo kama kupewa namba ya kupiga kwa maelezo zaidi ya 'link' ya kufuata.

Alisema kuwa kwa kufanya hivyo anaweka wazi mawasiliano yake ambayo ndugu, jamaa na marafiki watatafutwa na kuomba fedha au kuambiwa anadaiwa.

"Kwa sasa kuna wimbi kubwa na mwamko wa kukopa mtandaoni, wanaweka mtandaoni kwa sababu wanaficha masharti na riba zinazotozwa, wakati mwingine wanakuonesha kiwango cha rejesho ambacho ukikiweka kwa asilimia ni kubwa kuliko riba iliyoelekezwa na BoT.

"BoT hauwezi kuzuia mwamko wa ubunifu uliopo kwa sasa kwa kutumia teknolojia, bali inaweka utaratibu mzuri ili Watanzania wasiingie kwenye matatizo. Mikopo mtandaoni ni tatizo.

"Tunafuatilia 'applications' mbalimbali za mtandaoni wanaojitangaza wanatoa mikopo, lakini wengi hatuoni walioko nyuma wala masharti yake.

"Njia ya kudhibiti ni kutoa elimu kuhusu Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, hata ilivyoanza kutumika mwaka 2018 wapo walioikataa, lakini kadri siku zinavyosonga watu wanaikubali na kuishi kwenye taratibu, BoT haiingii kwenye soko kama askari, bali inaweka sheria kuelimisha wananchi na wenyewe watafuata utaratibu," alisema Mnyamani.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, BoT ilikuja na sheria hiyo baada ya kubani hakuna uwazi kwenye kukopesha watu, wakopaji kutojua kwa kina mkataba na wanapochelewesha marejesho hutozwa asilimia 50 ya rejesho na kwamba ipo kesi ya mtu alikopo Sh. milioni tatu na sasa deni limefika Sh. milioni 70.

Alisema mikopo imeumiza watu kwa kuwa baadhi wamepoteza mali zao, kuhama mji na wengine kupoteza maisha kutokana na kutozwa riba kubwa, na kwamba kisheria kama mtu anakopesha fedha bila leseni ya BoT, hana haki ya kudai fedha aliyokopesha.

"Kuna kampuni inatoa mikopo ya simu kwa mamalishe na bodaboda, mkataba wa ukopaji una kurasa 26 kwa lugha ya Kiingereza, mwishoni wengi wamejikuta wanatia saini kukubali.

"Ndio maana tunazikagua, tunaangalia kama mtoahuduma ana mfumo unaolinda na kushughulikia malalamiko ya wateja na kutoa elimu ya kifedha kwa wateja anaowakopesha.

Alisema kwa sasa, BoT inakusanya maoni ya wadau kwa ajili ya kuhuisha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ambayo baada ya kuanza kutumika walibaini baadhi ya vifungu vimekaa kibenki na kushindwa kutumika kwenye hali halisi.

Alisema ukusanyaji maoni ulianza Septemba na hadi Juni mwaka huu utakamilika kwa hatua za bungeni.

Alisema sheria imeweka madaraja ya huduma za kifedha ambazo ni benki ndogo, taasisi za fedha zisizo na amana, vyama vya akiba na mikopo (SACCOS) na VICOBA, lengo ni kuweka utaratibu wa uendeshaji sekta hiyo kwenye jamii.

Ofisa huyo alisema hadi Februari 9, mwaka huu tangu kuanza kwa sheria mwaka 2018, daraja la kwanza wako watatu ambao ni Vision Fund, Finca na Access Bank, daraja la pili waliopewa leseni ni 1,656 kati ya waombaji 2,274, SACCOS zilizopewa leseni ni 884 kati ya maombi 1,215 huku VICOBA maombi yakiwa ni 49,910 na waliopata leseni ni 48,826.

"BoT inafanya ukaguzi kwenye taasisi za fedha, hadi sasa 147 zimekaguliwa, lengo ifikapo Juni mwaka huu tuzifikie 200. Tunaangalia mtaji, mikopo iliyotolewa, madeni, uwazi na wapesi katika lugha ya mikataba kwa kuwa mingi inapungukiwa eneo hilo," alisema.

Mnyamani alisema ni muhimu kila mtu kabla ya kukopa kutafakari hatua tatu ambazo ni kutochukua mkopo bila kuwa na malengo mahususi, kukopa kwenye taasisi yenye leseni na kusoma na kuelewa vigezo na masharti yaliyowekwa.

Alisema BoT imekuja na sheria ambayo inamlinda mlaji kwa kuwa na kitengo cha kushughulikiwa malalamiko mbalimbali na kutaka wananchi kupeleka malalamiko ili hatua zichukuliwe ili kuhakikisha sekta ya fedha inakuwa tulivu muda wote.

Mnyamani alisema kwa mujibu wa kanuni, kuna aina mbili za riba ambazo ni 'flat interest rate' inayotozwa kwenye kiwango kilekile cha mkopo mwaka mzima na 'reducing balance' asilimia 10 mwezi wa kwanza, kisha wanatoza kwenye kiwango kilichosalia kadri mkopaji anavyopunguza.

"Kwa mujibu wa kanuni za kumlinda mlaji, ukokotoaji unaokubalika kikanuni ni huu wa kupunguza (reducing balance) kwa sababu 'flat rate' inaumiza zaidi. Wakopeshaji wengi hupenda 'flat rate' kwa sababu wanazozijua wenyewe," alibainisha.

# 1,500 hawajaripoti shuleni kuanza kidato cha kwanza

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

WANAFUNZI 1,507 kati ya 6,237 waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza na kupangiwa shule za sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, hawajaripoti shuleni.

Kaimu Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Wema Ayubu, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki alipoeleza kikao cha Baraza la Madiwani cha kupitia na kupitisha makadirio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25.


Alitoa taarifa hiyo baada ya kutakiwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo kufuatia swali la Diwani wa Kata ya Mtombozi, Yahaya Mfaume, aliyetaka kujua idadi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza walioripoti.

Akijibu swali hilo, Kaimu Ofisa Elimu huyo alisema wanafunzi waliochaguliwa kidato cha kwanza ni 6,237 na walioripoti hadi Februari 8, mwaka hu ni 4,730, sawa na asilimia 76.5 na wanafunzi 1,507 hawajaripoti. Mwisho wa kuripoti shuleni kisheria ni mwishoni mwa mwezi Machi, mwaka huu.

Katika hatua nyingine, Diwani wa Ngerengere, Kibena Kingo, alimwomba Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo na Menejimeti ya Halmashauri kuona umuhimu wa kuihamisha Shule ya Msingi Milengwelengwe kwa kuwa imo katika mkondo hatarishi wa mafuriko ya maji.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Lucas Lemomo, akijibu baadhi ya hoja za madiwani, alilimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya kuchukua hatua za haraka kukarabati shule hiyo.

Lemomo alisema hatua hiyo ni ya muda mfupi wakati mpango unaendelea kuomba mradi wa kuboresha elimu awali na msingi (BOOST) ili kujengwa shule mpya eneo la milimani.



# Diwani aamua kumlipa mwalimu anayejitolea kufundisha shuleni

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

DIWANI wa Kata ya Langai, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Jackson Leskar Sipitieck (Mugabe), amejitolea kumlipa Sh. 100,000 mwalimu wa Shule ya Msingi Langai ambaye anafundisha kwa kujitolea.

Pia diwani huyo maarufu kama Mugabe, ametoa trekta lake na kuwalimia ekari 10 kwenye shamba la shule, ili wanafunzi wa Shule ya Msingi Langai wapate kula chakula cha mchana shuleni.

Sipitieck akizungumza kwenye Kikao cha Kamati ya Shule ya Msingi Langai, alisema analipa Sh. 100,000 kwa mwalimu huyo, lengo likiwa kumwezesha mwalimu huyo anayejitolea kufundisha shuleni hapo.

"Baada ya kusikia changamoto ya mwalimu ambaye hajaajiriwa na serikali anayejitolea kufundisha watoto wetu, nikaona niwezeshe hilo ili kumpa motisha ya kufundisha zaidi," alisema Sipitieck.

"Watoto wengi wanatembea umbali mrefu kutoka nyumbani hadi shuleni hivyo wasipokuwa na chakula shuleni hawataweza kusoma vyema na kufaulu," alisema Sipitieck.

Mkazi wa kijiji hicho, Alais Moringe alimpongeza diwani huyo kwa kujitolea misaada hiyo kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wa Shule ya Msingi Langai wanasoma kwa bidii.

"Mheshimiwa Mugabe ni mtu wa maendeleo kwani ameona uchungu mwalimu wa kujitolea kuishi kwenye changamoto ya malipo ndipo akaamua kumsaidia na pia kuwalimia watoto ili wapate chakula," alisema Moringe.

Aliwataka wakazi wa Kata ya Langai kumpa ushirikiano wa kutosha diwani wao ili aweze kusimamia maendeleo na wao waone fahari ya kuwepo Simanjiro.

Alisema kumpata Diwani mwenye kudhubutu wa kujitolea kama huyo siyo jambo rahisi hivyo wanapaswa kumuunga mkono ili afanye maendeleo mengine zaidi.



Diwani wa Kata ya Magila, wilayani Muheza, mkoani Tanga, David Kilua (wa pili kulia), akitoa maelezo ya ujenzi wa madarasa sita, ofisi za walimu na jengo la utawala katika Shule ya Sekondari Magila juzi kwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wilayani humo. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, Salimu Sechambo, (wa tatu kulia) Diwani wa Viti Maalum, Mwajuma Semauya, (wa nne kulia) Diwani wa Kata ya Mhamba, Fatuma Msisi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Simanjiro yapitisha bajeti ya bilioni 39/-

**Na Cynthia Mwilolezi, SIMANJIRO**

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, wamepitisha Sh.bilioni 39 kwa ajili ya mapendekezo ya mpango wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025.

Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Happynes Masatu, akisoma bajeti hiyo, alisema itakidhi kwenye sekta mbalimbali ikiwamo afya, elimu, kilimo na mifugo.

Alisema bajeti hiyo imeandaliwa kwa kuzingatia mwongozo wa mpango wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2023/2024 na ilani ya uchaguzi ya CCM kwa mwaka 2020/2025.

Happynes alisema pia imelenga mpango wa maendeleo wa Taifa kwa miaka mitano, malengo ya maendeleo endelevu 2030 na dira ya Taifa kwa mwaka 2025.

Aidha, alisema katika sekta ya afya bajeti hiyo, itahakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya, katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya na kuhakikisha upatikanaji dawa na vifaa tiba.

"Katika sekta ya elimu tutahakikisha tunaboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwenye shule zote za msingi na sekondari kwa kujenga, kukarabati na kumalizia madarasa, mabweni, nyumba za walimu na vyoo," alisema Masatu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Baraka Kanunga, aliwasihi madiwani hao kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa watumishi wa halmashauri, katika utekelezaji wa bajeti hiyo.

"Twendeni tukatekeleze bajeti hii kwa manufaa ya wananchi wetu, kwani lengo ni kuhakikisha wanafanikiwa kupitia miradi itakayoanzishwa katika maeneo yao," alisema Kanunga.

Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alisema bajeti hiyo itawanufaisha wananchi wa eneo hilo, kwani kata nyingi zimeguswa katika sekta tofauti.

"Kupitishwa kwa bajeti ni hatua moja na kutekelezwa kwa bajeti ni hatua nyingine, hivyo madiwani na watumishi wapeane ushirikiano katika kufanikisha," alisema Ole Sendeka.

Diwani wa Kata ya Ruvu Remit, Yohana Maitei (Kadogoo), alisema bajeti hiyo ni ya matumaini katika sekta ya afya, elimu, kilimo na mifugo.

Diwani wa Kata ya Orkesumet, Sendeu Laizer, alisema anatarajia bajeti hiyo itaboresha zaidi miundombinu ya elimu, kwa kuwa iliyopita ilifanikisha ujenzi wa madarasa mapya ya Shule ya Sekondari Simanjiro.

Diwani wa Kata ya Loiborsoit, Siria Baraka Kiduya alisema bajeti ya mwaka huu imeinufaisha kata yake, kwa kuwa itapata madarasa mawili shule shikizi ya Songoyo na darasa moja Shule ya Msingi Losokonoi.

Diwani wa Kata ya Terrat, Jackson Ole Materi, alisema wananchi wa eneo hilo wameshapiga kura kwa Rais Samia Suluhu Hassan wanasubiria kudumbukiza kwenye boksi, kwani wamepata kituo cha afya na zahanati kila kijiji.

# TOSCI yaweka adhabu ukiukaji uuzaji mbegu

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

TAASISI ya kudhibiti ubora wa mbegu Tanzania (TOSCI) Kanda ya Kaskazini imesema wauzaji wa mbegu wanaokiuka sheria ya mbegu ya mwaka 2020 wanapaswa kufungwa jela miaka mitano mpaka miaka 12 na faini isiyozidi Sh. milioni 500.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki iliyopita na mkaguzi wa mbegu Kanda ya Kaskazini, Nicodemus Tlanka, wakati akizungumza na waandishi wa habari kwa ajili ya kuwajengea uwezo juu ya masuala ya mbegu.

Alisema mara nyingi makosa yanayofanywa na mawakala wa mbegu ni kuuza mbegu zisizo na nyaraka muhimu za manunuzi na uuzaji (risiti), kuuza mbegu zilizopitwa na wakati yaani miezi saba, kufungia vifungashio vya mbegu na kupima mbegu kwa kilogramu.

Tlanka alitaja makosa mengine kuwa ni kuuza mbegu ambazo hazina lebo ya TOSCI na kuweka mbegu sakafuni au kuchanganya na mbolea au bidhaa nyingine.

Aidha, alisema adhabu wanazotoza TOSCI muuzaji anapokutwa na kosa ni onyo, kufutiwa kibali cha kujihusisha na mbegu na kushtakiwa kwa mujibu wa sheria.

Mkaguzi wa mbegu kutoka TOSCI, Frank Maximilian alisema mbegu bora sifa zake ni mbegu halisi, usafi, uotaji na afya ya mbegu.

Alisema zinatakiwa kupimwa kila baada ya miezi saba hivyo wauzaji wanatakiwa kuzingatia hilo ili mbegu ziendelee kuwa na ubora wakulima wasije kuuziwa mbegu mbovu.

Kwa upande wake Meneja Mwandamizi wa Taasisi ya kuboresha mifumo ya masoko (AMDT), Mary Kalavu alisema wanaangalia mnyororo wa thamani kwa mazao ya alizeti na mikunde na wanatoa elimu kwa wakulima kwa kushirikiana na wadau.

Meneja huyo alisema mbegu bora wanahakikisha zinawafikia wakulima na wameweza kuwapatia elimu maofisa ugani zaidi ya 100.

Aliongeza kuwa AMDT kwa kushirikiana na TOSCI wanatoa elimu ya mbegu kwa wakulima katika mikoa 12.





# Wakulima waomba elimu ya uchanganyaji viwatilifu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA wa pamba mkoani Shinyanga, wameomba kupewa elimu juu ya namna sahihi ya kuchanganyanga dawa za viwatilifu kukabiliana na wadudu ambao hawafi pindi wanapopulizia dawa hizo shambani hali inayopunguza uzalishaji katika zao hilo.

Wametoa ombi hilo kwa nyakati tofauti wakati wa ulipaji wa malipo ya pili ya zao hilo kwa wakulima waliokiuzia Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) zaidi ya kilo milioni 5.1 katika msimu wa 2023/2024 ambapo kilo moja wanalipwa Sh.36 sawa na zaidi ya Sh.milioni 186.316 iliyotolewa.

Mmoja wa wakulima hao kutoka AMCOS ya Isanjabadugu-Ushetu Jumanne Gwesa alisema, wamekuwa wakishindwa kujua sababu kwa nini viwatilifu hivyo vimekuwa vikishindwa kuua wadudu kwenye pamba na endapo wangekuwa na elimu sahihi wangezalisha zaidi ya sasa.

Katibu wa Chama cha Msingi Gimagi-Kishapu, Raphael Mongo alisema, ili kuendelea kuyafikia malengo ya uzalishaji wa zao hilo kila mwaka ni vema maaofisa ugani waliopo kila kata kuhakikisha wanawatembelea na kuwapatia elimu sahihi wakulima hao.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, aliwataka maofisa ugani wote ngazi za kata kuwatembelea wakulima wa zao hilo na kuwaelimisha njia sahihi ya uchangangaji wa viwatilifu ili kudhibiti wadudu wanaoshambulia pamba na kuongeza uzalishaji na sio kushinda wamekaa maofisini tu.

Alisema, mkoa umepokea kiasi cha Sh. bilioni 27 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya kilimo ikiwamo ujenzi wa mabwawa makubwa mawili ya kilimo cha umwagiliaji na kununua pikipiki 224 za maaofisa ugani ambao watakuwa wanawatembelea wakulima na kuwapatia elimu ya namna ya kulima kisasa nasio vinginevyo. Awali akitoa taarifa ya utoaji wa malipo ya pili Mwenyekiti wa KACU Tano Nsabi alisema, utoaji wa malipo ya pili ulianza msimu wa kilimo 2019/2020 chini ya aliyekuwa Mwenyekiti Emmanuel Charahani na msimu huu wanatoa malipo ya pili Sh.36 kwa kila kilo moja na msimu ujao watalipa zaidi kulingana na faida watakayokuwa wameipata.

Mrajisi Msaidizi Mkoa wa Shinyanga, Hilda Boniphace, alisema, kitendo cha ushirika huo kujitosa na kununua pamba kimesababisha kuwapo kwa ushindani wa bei na kampuni nyingine na kuongeza uzalishaji pia mwakani msimu uliopita mkoa ulizalisha kilo milioni 10.4 na sasa umezalisha kilo milioni 38.



Mkuu wa Wilaya ya Rorya, mkoani Mara, Juma Chikoka (kushoto), akipokea madawati 150 kwa ajili ya Shule ya Msingi Minigo kutoka kwa Kaimu Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Hamadan Silliah, pia madawati 100 yalitolewa na benki hiyo kwa Shule ya Msingi Nyanduru, mabati 168 kwa Shule ya Girango, mabati 100 kwa Shule ya Sekondari Prof. Sarungi na ukarabati wa madarasa 7 ya Shule ya Msingi Minigo, msaada wote una thamani ya Sh. milioni 84. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Akamatwa kwa wizi alama za barabarani

**Na Halima Ikunji,** TABORA

JESHI la Polisi mkoani Tabora limemkamata Moshi, kwa tuhuma za uharibifu na wizi wa alama za usalama barabarani kutoka katika barabara mbalimbali katika mkoa huo baada ya kukutwa na alama zenye thamani ya zaidi ya Sh.milioni 10 nyumbani kwake.

Akitoa taarifa hiyo kwa waandishi wa habari Kamanda wa Polisi, ACP Richard Abwao, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa saa 12 asubuhi katika Kata ya Usege wilayani Kaliua.

Alisema walimkamata mtuhumiwa huyo baada ya kupata taarifa kutoka kwa wasamalia wema katika ambao wanapiga vita vitendo vya uharibifu wa alama za barabarani.

Kamanda Abwao alisema upelelezi wa kina unaendelea dhidi ya tuhuma hizo na watamtumia mshtakiwa huyo kuutambua mtandao wote wa wahalifu waliohusika katika kung'oa alama hizo za barabarani.

Hata hivyo mshtakiwa huyo alipofikishwa mbele ya Kamati ya Usalama Mkoa ili kueleza mtandao wake na wapi wanapeleka alama hizo alikana kuwa kuhusika wa moja kwa moja kwa madai kuwa zililetwa na kuhifadhiwa nyumbani kwake na mtu aliyemtaja kwa jina moja la Musa, mfanyakazi wa kampuni ya kichina inayojihusisha na ujenzi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Buriani, alisema mpaka sasa alama 428 za barabarani zimeondolewa katika barabara za mkoa huo jambo linaloitia serikali hasara. Dk. Batilda alisema wakati serikali inapambana na kujenga miundombinu ya barabara lipo kundi kubwa la watu ambao wanaiharibu miundombinu ya barabara bila kuogopa kama itaweza kuwaletea matatizo. Aidha, aliliagiza jeshi hilo limsake na kumhoji mtuhumiwa huyo aliyetajwa na pia kuendelea kumhoji huyo aliyekamatwa ili kusaidia kupata mtandao mzima wa wizi wa alama hizo.

Baadhi ya Wakazi wa Kata hiyo akiwamo Alli Juma walilaani kitendo hicho cha uharibifu wa miundombinu na wizi wa alama zilizowekwa kwa ajili ya usalama wa wananchi na kuahidi kutoa ushirikiano kuhakikisha wote wanakamatwa ili wachukuliwe hatua zaidi ikiwamo kufikishwa mahakamani.

# Wachuuzi choroko, dengu rumbesa wapigwa 'stop'

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amepiga marufuku wachuuzi wanaonunua mazao ya choroko na dengu kwa wakulima mashambani kwa vipimo vya rumbesa kinyume cha sheria na kuvitaka vyama vya ushirika kuimarisha mfumo wa stakabadhi ghalani ili kumkomboa mkulima kiuchumi.

Mndeme alitoa marufuku hiyo juzi wakati akifungua kikao cha wadau wa mfumo wa stakabadhi ghalani na kutaja mfumo huo kuwa utachangia katika kuongeza uzalishaji wa mazao, ambapo mkulima atapata fursa ya kuuza mazao yake kwa bei yenye faida na shindani kupitia mnada.

"Mfumo huu wa stakabadhi ghalani mazao yatakuwa yakiuzwa kwa njia ya mnada kwa kuwa na ushindani zaidi kwa wafanyabiashara, hali ambayo italeta uvumbuzi wa bei zenye tija kwa wakulima, mfano zao la korosho katika mikoa ya Lindi na Mtwara bei imeimarika msimu hadi msimu na hii ni kutokana na matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani," alisema Mndeme.

Alisema utekelezaji wa mfumo huo utasaidia pia serikali kupata mapato, pamoja na wakulima kupata taarifa na takwimu mbalimbali za mazao kwa wakati na usahihi, pamoja na kuchochea huduma za kifedha vijijini, ambapo wakulima malipo na manunuzi yatapitia kwenye taasisi za kifedha.

Naibu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na Udhibiti kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Collins Nyakunga, alisema mfumo huo utaleta uwazi kwani utakusanya mazao na kuyapeleka kwenye masoko na kubainisha kwamba kwa nchi nzima kuna jumla ya Vyama vya Ushirika 7,391 na AMCOS 4,475 na jumla ya wanachama milioni 12.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, Asangye Bangu, alisema mfumo huo utaleta bei ya ushindani kupitia mnada na wakulimwa watalipwa pesa zao ndani ya siku tatu.

Nao baadhi ya wakulima wa mazao ya mikunde akiwamo, Lucas Dogani, alisema mfumo huo wa mauzo ya mazao stakabadhi ghalani ni mzuri kwani utawasaidia kupata fedha nyingi kulingana na mavuno yaliyopata na siyo kulanguliwa tena na wafanyabiashara wanaotumia vipimo vya rumbesa.

Nipashe
Spotika




USAJILI WA DIRISHA DOGO ULIOANZA KULIPA LIGI KUU UK. 14



Cristiano Ronaldo

# WACHEZAJI 10 AMBAO WANGENOGESHA AFCON

**ABIDJAN, Ivory Coast**

KOMBE la Mataifa ya Afrika (Afcon), ni michuano yenye hadhi inayoonyesha vipaji bora vya soka kutoka barani humu. Kwa miaka mingi, wachezaji kadhaa wenye asili ya Kiafrika wametoa mchango mkubwa kwenye jukwaa la kimataifa, wakiwakilisha nchi wanazostahiki kulingana na urithi wao.

Hata hivyo, kuna baadhi ya majina ya wachezaji mashuhuri ambao wangeweza kustahili kucheza Afcon, lakini hatimaye wakachagua njia tofauti.

Hapa, tunawaangalia wachezaji 10 kama hao ambao wangeweza kustahiki kucheza Kombe la Mataifa ya Afrika kulingana na uhusiano wao wa kifamilia na urithi...

**Bukayo Saka**

Winga huyo Mwingereza mwenye umri wa miaka 22, ameibuka kuwa mchezaji muhimu kwenye kikosi cha Gareth Southgate cha Timu ya Taifa ya England. Licha ya kuzaliwa London, Bukayo Saka angeweza kuwa mchezaji wa Timu ya Taifa ya Nigeria kutokana na asili yake ya Nigeria. Wazazi wake, ambao wana asili ya Nigeria, walimpa jina la Kiyoruba, ambalo tafsiri yake ni "Ongeza kwa furaha."

**Curtis Jones**

Mchezaji mwingine mwenye kipaji na uzazi wa Nigeria ni Curtis Jones, ambaye kwa sasa anacheza katika Klabu ya Liverpool. Akiwa na umri wa miaka 23, Jones angeweza kuimarisha safu ya kiungo ya Nigeria kwenye Kombe la Mataifa ya Afrika, kwani wazazi wake wana asili ya Nigeria.

**William Saliba**

Beki huyo wa Ufaransa, ambaye kwa sasa anaichezea Arsenal, ana uhusiano wa kifamilia na Cameroon kupitia kwa mama yake. Licha ya kuiwakilisha Ufaransa katika kiwango cha kimataifa, Saliba angeweza kuwa kiungo wa ulinzi wa Timu ya Taifa ya Cameroon katika michuano ya Afcon.

**Ibrahima Konate**

Kama Saliba, Ibrahima Konate ni mchezaji wa mpira wa miguu wa Ufaransa aliyezaliwa na wazazi wa Kiafrika. Kwa urithi wa Mali, Konate angeweza kutoa nguvu na uimara kwa safu ya ulinzi ya Mali katika Kombe la Mataifa ya Afrika.

**Kylian Mbappe**

Kylian Mbappe, mmoja wa vipaji vya kuvutia zaidi katika soka duniani, ana sifa mbili kutokana na asili ya wazazi wake. Akiwa na baba Mcameroon na mama wa Algeria, Mbappe angeweza kuwa mchezaji mahiri kwa taifa lolote kati ya hayo mawili katika Kombe la Mataifa ya Afrika.

**Nico Williams**

Wakati kaka yake, Inaki Williams, alichagua Ghana badala ya Hispania, Nico Williams alichagua kuiwakilisha Hispania kimataifa. Mzaliwa wa Hispania, Nico alikuwa na chaguo la kuichezea Ghana kutokana na urithi wake lakini aliamua vinginevyo.

**Alphonso Davies**

Akiwa amezaliwa nchini Ghana kwa wazazi wakimbizi wa Liberia, Davies angechagua kuchezea Ghana au Liberia kwenye Kombe la Mataifa ya Afrika. Hata hivyo, alichagua kuwakilisha Canada, ambako amepata mafanikio makubwa. Kasi na ustadi wake ungeweza kubadilisha mchezo kwa Ghana au Liberia kwenye Afcon.

**Romelu Lukaku**

Romelu Lukaku, mshambuliaji mahiri wa Ubelgiji, angeweza kushiriki Afcon akiwakilisha Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Mzaliwa wa wazazi wa Congo nchini Ubelgiji, babake Lukaku, Roger Lukaku, aliiwakilisha Zaire kimataifa. Lakini Romelu alichagua kuiwakilisha Ubelgiji, ambapo kwa sasa ndiye mfungaji bora wa muda wote.

**Karim Benzema**

Kabla ya kuiwakilisha Ufaransa, Karim Benzema alikuwa akiwaniwa na Shirikisho la Soka la Algeria. Akiwa na wazazi wa Algeria, Benzema alikuwa na chaguo la kuiwakilisha Algeria katika Kombe la Mataifa ya Afrika, lakini hatimaye alichagua kuendeleza soka yake ya Kimataifa na Ufaransa.

Mfikirie akiwa pamoja na Riyad Mahrez, akiweza kutengeneza kundi la washambuliaji wawili bora kwenye Afcon.

**Cristiano Ronaldo**

Wakati Cristiano Ronaldo amepata hadhi ya hadithi na Ureno, angeweza kustahili kuichezea Cape Verde kupitia kwa bibi yake. Urithi wake wa Kiafrika kutoka Cape Verde unaongeza mwelekeo wa kuvutia kwa kazi yake ya kifahari, na angeweza kuwa ishara ya kujivunia kwa Cape Verde, uwezekano wa kuinua viwango vyao vya Afcon

Wachezaji hawa 10 wanawakilisha sehemu ya kundi la vipaji ambalo lingeweza kupamba shindano hilo la hadhi ya kandanda barani Afrika. Ingawa wamefanya vema katika uwakilishi wa mataifa mengine, urithi wao na uhusiano wa kifamilia ungeweza kuwafanya watoe rangi za nchi mbalimbali za Afrika katika michuano hii ya kifahari.

Hatimaye, chaguo zao zinaonesha utambulisho, utii na fursa katika ulimwengu wa soka la kimataifa.

## ISIKUPITE

BAO alilofunga Mohamed Salah wakati Liverpool ikiichapa Brentford mabao 4-1 juzi, sasa anakuwa amefunga na kusaidia (assists) katika mechi 30 tofauti za Ligi Kuu England. Ni Wayne Rooney (36), Thierry Henry (32) na Alan Shearer (31) pekee ndio wamefanya hivyo mara nyingi zaidi yake.



# MATAIFA 10 BORA YALIYOCHEZA MARA NYINGI FAINALI YA AFCON


Rais wa Ivory Coast, Alassane Ouattara na nahodha wa timu ya taifa hilo, Max Gradel, wakinyanyua Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023, baada ya nchi hiyo kulitwaa katika mechi ya fainali dhidi ya Nigeria Februari 13, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

XAVI

**ABIDJAN, Ivory Coast**

MICHUANO ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), inasimama kama moja ya mashindano ya hadhi ya juu zaidi katika kandanda ya Afrika, ikionesha vipaji vikubwa vya bara hili na shauku ya mchezo huo mzuri.

Kwa miaka mingi, mataifa kadhaa yameweka alama katika historia ya Afcon, huku baadhi yao wakionja utamu wa ushindi na wengine kustahimili machungu ya kushindwa.

Hapa tunatazama mataifa 10 bora yaliyotinga hatua ya fainali ya michuano ya Afcon mara nyingi zaidi na tunaangalia safari yao ya ushindi na huzuni.

**Senegal - Mara 3**

'Simba wa Teranga', Senegal imecheza mechi tatu za fainali katika michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika na hivyo kudhihirisha kuibuka kwao kama kinara wa soka barani Afrika. Wakati harakati zao za kusaka ubingwa wa Afcon, safari ya Senegal imekuwa na uthabiti na matamanio, na kudhihirisha ari ya soka la Afrika.

**Sudan - Mara 3**

Safari ya soka ya Sudan imewashuhudia wakipamba hatua ya fainali ya Afcon mara tatu, wakionesha ari yao na kujitolea kwa mchezo huo. Ingawa ushindi wao umekuwa mdogo, uwapo wa Sudan kwenye fainali unaonesha uthabiti na uthubutu wao katika kukabiliana na hali ngumu, unaojumuisha ari ya soka la Afrika.

**Tunisia - Mara 3**

'Tai wa Carthage', imepanda imecheza fainali tatu za mwisho katika Kombe la Mataifa ya Afrika, na kudhihirisha uwapo wao wa kudumu katika soka la Afrika. Licha ya uchezaji wao mfululizo, Tunisia imekumbwa na huzuni, ikiwa ni pamoja na kushindwa kwao katika fainali ya 1965.

**Zambia - Mara 3**

Chipolopolo ya Zambia imecheza mechi tatu za fainali katika michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika, ikionesha uthabiti na ari yao katika hatua ya bara.

Wakati wao wa kutwaa taji ulikuja mwaka 2012, hata hivyo, safari yao pia imekumbwa na huzuni, hasa kushindwa kwao katika fainali za 1974 na 1994.

**Algeria - Mara 3**

Mbweha wa Jangwani wa Algeria wameacha alama isiyofutika kwenye Afcon kwa kutinga hatua ya fainali mara tatu na kuhitimisha kwa ushindi wao wa ubingwa mnamo mwaka 1990 na 2019. Mchanganyiko wa ustadi na uthubutu wa Timu ya Taifa ya Algeria umewafanya wafikie kilele cha soka la Afrika.

Hata hivyo, katikati ya ushindi wao kuna uchungu wa huzuni, uliodhihirishwa na kushindwa kwao kwa uchungu katika fainali ya 1980.

**Ivory Coast - Mara 5**

Tembo wa Ivory Coast wameonesha umahiri wao katika soka la Afrika kwa kucheza mara tano katika hatua ya fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika, huku mechi yao ya hivi karibuni ikiwa dhidi ya Super Eagles, Nigeria na kulitwaa taji hilo.

Wakiwa na mataji mawili ya ubingwa kwa jina lao, ikiwa ni pamoja na ushindi wao wa kihistoria mwaka 2015, Ivory Coast imeibuka kuwa nguvu ya kuhesabiwa katika hatua ya bara. Hata hivyo, safari yao imechoshwa na huzuni, ikidhihirishwa na kushindwa kwao katika fainali ya 2012.

**Cameroon - Mara 7**

Simba wasiofugika, Cameroon wamenguruma kwenye hatua ya fainali ya Afcon mara saba na kutwaa ubingwa mara tano. Kuanzia ushindi wao wa kwanza mwaka 1984 hadi ushindi wao wa mwaka 2017, uthabiti na ukakamavu wa Cameroon umewafanya kuwa na nguvu kubwa katika soka la Afrika.

Hata hivyo, safari yao pia imekumbwa na huzuni nyingi, ikiwa ni pamoja na kushindwa kwao katika fainali za mwaka 1986 na 2002.

**Nigeria - Mara 8**

'Super Eagles', Nigeria imekuwa na nguvu kubwa katika soka la Afrika, ikicheza mara nane katika hatua ya fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika. Waliingia fainali katika michuano ya Afcon ya mwaka huu na wakafungwa na Ivory Coast. Wakiwa na mataji matatu ya ubingwa kwa sifa zao, ikiwa ni pamoja na ushindi wao wa kukumbukwa mwaka 1980, 1994 na 2013, Nigeria imeimarisha hadhi yake kama ngome ya bara.

Hata hivyo, katikati ya ushindi wao, Super Eagles wamevumilia nyakati za huzuni, kama vile kushindwa kwao katika fainali za 1988, 1990 na 2000, kutumikia kama ukumbusho wa hali isiyotabirika ya soka.

**Ghana - Mara 9**

'Black Stars', Ghana wametamba katika hatua ya fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa mara tisa, wakionesha uwapo wao wa kudumu katika soka la Afrika. Wakiwa na mataji manne ya ubingwa kwa jina lao, ikiwa ni pamoja na ushindi wao wa kihistoria wa mwaka 1963 na 1965, Ghana imeacha alama isiyofutika kwenye michuano hiyo.

Hata hivyo, licha ya ubora wao thabiti, Black Stars pia wamepatwa na huzuni, haswa katika kushindwa kwao katika fainali za mwaka 2010 na 2015, na kuwaacha wakitamani ladha nyingine ya utukufu wa Afcon.

**Misri - Mara 10**

Urithi wa soka wa Misri ni sawa na utukufu wa Afcon na mechi kumi za fainali. 'Mafarao' wameshinda mara saba taji hilo, na kujiweka kama taifa lenye mafanikio zaidi katika historia ya kombe hilo.

Kuanzia ushindi wao wa kwanza mwaka 1957 hadi kichapo cha mwaka 2021, utawala wa Misri katika soka la Afrika hauna mpinzani. Hata hivyo, katikati ya ushindi wao kuna nyakati za huzuni, ikiwa ni pamoja na kushindwa kwao katika fainali ya 1962 na 2017.

Kuanzia nyakati za ushindi hadi kushindwa kwa kuhuzunisha moyo, mataifa haya 10 bora yamepitia wigo kamili wa hisia kwenye hatua kuu ya soka la Afrika. Wanapoendelea kujitahidi kupata utukufu, hadithi zao zitatia moyo vizazi vijavyo na kutukumbusha moyo wa kudumu wa mchezo huo mzuri.

## Nukuu

"Kwa wakati huu, nadhani Arsenal. Msimu huu, itakuwa karibu sana. Nafikiri wanaweza kufanya hivyo," **Nyota wa zamani wa Chelsea, Petr Cech, anaamini Arsenal wanaweza kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu dhidi ya Liverpool na Manchester City.**



"Liverpool, kwangu, ndio wapinzani wa karibu zaidi kwa sababu kuna baadhi ya michezo ambayo Liverpool hawajacheza vizuri, lakini wamepata matokeo. Arsenal inabidi wacheze vizuri ili kushinda na wasipocheza vizuri, wanaweza wasishinde na ndiyo maana hata wanavyofanya vizuri sasa bado nadhani ni kati ya Man City na Liverpool," **Mchambuzi wa soka, John Barnes, akieleza kwa nini anadhani Liverpool ina nafasi zaidi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu kuliko Arsenal.**



"Kwangu mimi, ni kosa kubwa zaidi katika uongozi wake na katika historia ya kisasa ya klabu. Messi angeweza kuwa sehemu ya suluhu na hatujui gharama ya michezo ambayo ilimaanisha kwa Barca," **Rais wa zamani wa Barcelona, Victor Font, akimlaumu rais wa sasa wa klabu hiyo, Joan Laporta namna alivyoshughulikia vibaya suala la Lionel Messi.**





Mudathir Yahaya, akishangilia moja ya mabao yake kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

# MUDATHIR ALIVYOGEUKA SHUJAA MPYA YANGA

**Na Adam Fungamwango**

KWA siku za karibuni, kiungo mkabaji wa Yanga, Mudathir Yahaya, amekuwa mkombozi wa baadhi ya mechi zinazoonekana kuwa ngumu kwa timu hiyo.

Mchezaji huyo aliyesajili kipindi cha dirisha dogo la msimu wa 2022/23, amekuwa msaada mkubwa kwa Yanga, akifunga mabao katika mechi ambazo baadhi ya wanachama na mashabiki wa Yanga wakiwa wameshaanza kukata tamaa.

Tangu kuondoka kwa straika Fiston Mayele, kiungo huyo ambaye alisajili akiwa hana timu yoyote baada ya kuachana na Azam, ndiye amekuwa tegemeo katika ufungaji, hasa katika mechi ngumu.

Kwa mara nyingine tena, juzi alifunga mabao mawili dhidi ya KMC, Yanga ikishinda 3-0. Mudathir amefunguka juu ya staili yake ya kushangilia kama vile anapiga simu.

"Ishara ya kuwapigia ndugu zangu nyumbani, najua wananiona kwenye televisheni, na wao wanafurahi sana wakiniona nimefunga, na nadhani msimu huu nimekuwa na bahati sana kwenye ufungaji," alisema Mudathir ambaye ameshapachika mabao sita kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na matano yamekuwa muhimu zaidi, na ya kuamua matokeo.

Bao lake la kwanza alilifunga Agosti 23, mwaka huu katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, Yanga ikiishindilia KMC 5-0.

Hata hivyo, halikuwa bao muhimu sana kwa sababu liliongezea tu idadi ya mabao.

Katika makala haya tunakuletea mabao matano ya mchezaji huyo ambayo yameiwezesha Yanga kufika hapo ilipo.

**Yanga 1-0 Namungo**

Zilibaki dakika tatu tu mechi kati ya Yanga na Namungo iliyokuwa ikichezwa Azam Comoplex, imalizike. Baadhi ya wanachama na mashabiki walikuwa wameshataka tamaa. Mudathir aliingia dakika ya 68 akichukua nafasi ya Pacome Zouzoua.

Dakika tatu tu kabla mechi kumalizika, alipachika bao pekee, akiunganisha kwa mguu wa kulia krosi ya Yao Kouassi kutoka wingi ya kulia, Yanga ikiondoka na ushindi wa bao hilo pekee, Septemba 30, mwaka jana.

**Yanga 1-0 Dodoma Jiji FC**

Kwenye uwanja huo huo wa Azam Complex, Februari 5, mwaka huu, kiungo huyo alifanya tena kama ilivyokuwa katika mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Namungo. Aliingia kipindi cha pili, safari hii akichukua nafasi ya Jonas Mkude.

Dakika nne kabla ya mechi kumalizika, zikionekana kabisa dalili za sare dhidi ya Dodoma Jiji, aliukwamisha mpira wavuni, safari hii akipata krosi kutoka kwa Nickson Kibabage kwenye wingi ya kushoto.

**Yanga 2-1 Mashujaa FC**

Siku tatu baadaye, Februari 8, mwaka huu, Yanga ilicheza tena mechi ya Ligi Kuu, Uwanja wa Azam Complex dhidi ya Mashujaa. Dakika tano kabla ya mechi hiyo kumalizika ubao ukiwa unasomeka 1-1, lakini wakati sare ikionekana kutokea, kama kawaida yake, Mudathir aliuweka ndani ya kamba mpira wa krosi iliyopigwa kutoka wingi ya kulia na Kennedy Musonda na kuipa Yanga ushindi.

**Yanga 3-0 KMC**

Ilionekana kama vile Mudathir ni mfalme wa Chamazi pekee, lakini kumbe sivyo. Juzi kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro, sekunde ya 54 tu akapachika bao la kwanza dhidi ya KMC.

Lilikuwa ni bao jepesi tu Clement Mzize akifanikiwa kuupokonya mpira waliokuwa wakipasiana kizembe mabeki wa timu hiyo na kipa wao, Wilbol Maseke, akampa Mudathir ambaye alipiga shuti kali lililowababatiza mabeki, ukamrudia Stephane Aziz Ki, ambaye naye alijaribu, kipa aliupangua, ukaenda kuangukia tena kwa kiungo huyo kabla ya kuupachika wavuni kiulaini, bao ambalo liiwachanganya wachezaji wa KMC, kiasi cha kupigana wenyewe kwa wenyewe.

**Yanga 3-0 KMC**

Katika mechi hiyo hiyo, alipachika bao la pili dakika ya 53, alipoutokea mpira wa krosi iliyopigwa na Kibabage, wakati mabeki wa KMC wakiusubiri wauokoe, mfungaji alitoka nyuma yao na kuukwamisha wavuni kirahisi kwa mara nyingine, kirahisi sana.

Lilikuwa ni bao la pili ambalo liliwamaliza nguvu kabisa KMC.

**JE, WAJUA?**



BAO alilofunga Kylian Mbappe juzi wakati Paris St-Germain ikishinda 2-0 kwenye Ligue 1 dhidi ya Nantes, kufikisha mabao 21 kwenye ligi hiyo msimu huu. Kwa ujumla, ana mabao 244 na asisti 93 katika mechi 290 alizoichezea PSG na ameisaidia klabu hiyo kushinda mataji matano ya Ligue



# Dodoma Jiji yatangaza bomoabomoa ujenzi holela

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetangaza kuanza kubomoa vibanda vya biashara vilivyojengwa kinyume na utaratibu na kuwachukulia hatua kali kisheria, huku ikitoa siku tatu kuanzia leo kubomoa kwa hiari yao.

Pia, ubomoaji huo utahusisha kuvunja makazi yaliyojengwa kinyume na utaratibu, kanuni na sheria za mipango miji.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Fungo, alisema walishatoa elimu kuhusu wananchi kufuata sheria ya mipango miji na kuwataka ndani ya siku saba kuanzia sasa wawe wamebomoa wenyewe.

"Watakaokaidi watalipa gharama za ubomoaji na tozo la kukaidi amri halali ya serikali,"alisema.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara wanaofanya biashara kando ya masoko kutofanya biashara kwenye maeneo hayo ambayo tayari yalishazuiliwa.

Fungo alisema kuwa zoezi hilo linafanyika kutokana na baadhi ya maeneo ya wazi na yale yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji wa miundombinu mbalimbali wananchi wamevamia na kuanza kujenga makazi yao bila kufuata sheria za mipango miji.

"Halmashauri ya Jiji la Dodoma ilishatoa angalizo la kuwataka wananchi kujiepusha na uvujaji wa sheria kwa kujenga holela pamoja na kuwataka pia wafanyabiashara kutofanya biashara kwenye maeneo yasiyoruhusiwa, ikiwemo kandokando ya barabara,pembezoni mwa majengo ofisi,"alisema.



Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga wakiwa kwenye kikao cha Baraza cha Robo ya Pili ya mwaka wa fedha 2023/2024 na kulalamikia mfumo mpya wa Tausi wa ukusanyaji mapato, kuwa unakwamisha halmashauri kukusanya mapato yake kwa wafanyabiashara kutokana na kugoma kusoma, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wananchi watakiwa kujitokeza kuchanja

**Renatha Msungu na Thobias Mwanakatwe**

WANANCHI wametakiwa kuhakikisha watoto wenye umri wa miezi tisa hadi chini ya umri wa miaka mitano wanapatiwa chanjo ya surua na Rubella, ili kuwakinga na mlipuko wa magonjwa.

Akizungumza katika uzinduzi wa kampeni ya kitaifa ya chanjo hiyo, Kaimu Mkurugenzi Huduma za Kinga kutoka Wizara ya Afya Dk. Tumaini Haonga alisema wananchi wahakikishe wanawapeleka watoto kupatiwa chanjo kwa kuwa ni salama na zimethibitishwa, ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza kwa kutokupatiwa chanjo.

"Chanjo ipo naomba wananchi wenye watoto wa umri huo wawapeleke kupata chanjo zinapatikana nchini kote kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali. Tunatarajia kuwafikia watoto 8,980,810,"alisema.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto (UNICEF), Dk. John George, aliipongeza serikali kwa kuzindua kampeni ya utoaji wa chanjo huku akiwataka kuendeleza utoaji elimu ya umuhimu wa chanjo hiyo kwa jamii.

Mratibu wa Mpango wa Chanjo kutoka TAMISEMI, Dk. Joseline Ishengoma alisema serikali haitachoka kufuatilia watoto kwenda kupata chanjo na kutakuwa na kliniki tembezi ili kila mtoto mwenye umri huo afikiwe.

Wakati huo huo, jumla ya watoto 261,594 wenye umri huo mkoani Singida wanatarajia kupewa chanjo kupitiwa kampeni hiyo. Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, alisema Mkoa wa Singida ulipata mlipuko wa ugonjwa wa surua rubella kuanzia Februari hadi Oktoba mwaka jana katika halmashauri za Itigi, Ikungi, Singida, Mkalama na Iramba na watoto 345 walipata ugonjwa huo.

"Ugonjwa huu unaweza kumpata mtu mwenye rika na umri wowote lakini watoto chini ya miaka mitano wapo kwenye hatari zaidi ya kupata ugonjwa huo, hivyo chanjo dhidi ya ugonjwa wa surua na rubella itatokewa katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa mtoto nwenye unribwa miezi tisa dozi ya kwanza na akiwa na miezi 18 atapata dozi ya pili," alisema.

Dk.Mganga alisema mkoa umesambaza chanjo zote dhidi ya ugonjwa wa surua na Rubella hadi ngazi ya kituo cha kutolea huduma za afya na vifaa mbalimbali vya chanjo ambapo kampeni hiyo pia itatolewa kwenye shule, vituo vya mabasi na katika ofisi za vijiji na mitaa. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmshauri ya Iramba, Michael Matomora alisema kuwa Iramba pekee inatarajia kuchanja watoto elfu 43,218.

# Wanaofuja fedha za yatima waonywa

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WAMIILIKI wa vituo vya kulelea jamii wameaswa kuacha tabia ya kutumia misaada inayotolewa na wahisani kujinufaisha wao wenyewe badala yake wafikishie kwa walengwa.

Meneja wa Kampuni ya Jumaco Property LTD inayojishughulisha na upimaji na uuzaji wa viwanja na kusaidia jamii, Sabinusi Mathew alitoa rai hiyo baada ya kukabidhi misaada mbalimbali kwenye kituo cha Nyumba ya Matumini kilichopo Miyuji Dodoma.

Alisema ni muhimu wamiliki wa vituo hiyo wanapaswa kutotumia nafasi hiyo kwa kujipatia mali na fedha zinazotolewa na wasamaria wema kwa kupitia migongo ya watoto hao ambao wanaostahili kusaidiwa ili kupata haki zao za msingi.

Mathew aliomba serikali kuchunguza zaidi vituo hivyo kwa kuwa vilivyo vingi vipo kwenye mikoba ya wamiliki na wanatumia misaada kujinufaisha wenyewe.

Alisema kuna ulazima mkubwa serikali kuchukua hatua zaidi za kisheria za kuwachunguza walimiki hao, ili kuwatambua kama vituo vyao vina usajili na vinatambuliwa na wana sifa ya kuwalea watoto hao wenye kutakiwa kusaidiwa.

"Ninaiomba serikali kwa kushirikiana na halmashauri zetu kuwachunguza hao wamiliki wa vituo hivyo kama vituo vyao vimepata usajili na vina vigezo, ili kuwabaini misaada mbalimbali inayotolewa na serikali, watu binafsi, taasisi za dini, na mashirika yasiyo ya kiserikali kama inawafikia walengwa husika,"alisema.

Meneja huyo alisema kampuni hiyo imekuwa ikisaidia jamii isiyojiweza ikiwemo vituo mbalimbali, ili watoto wapate haki zao za msingi kama watoto wengine wenye wazazi au walezi.

Mkuu wa Shirika la Mtakatifu Ursula wa Moyo wa Yesu Mteswa Miyuji, Modesta Temu alisema kuwa misaada inayotolewa imekuwa ikisaidia kutatua kwa baadhi ya matatizo yanayowakabili watoto hao, ikiwemo kwenye afya, elimu, mavazi, chakula, maji na umeme.

Mkuu huyo huyo alisema kuwa msaada uliotolewa na kampuni hiyo utasaidia kutatua matatizo hayo.



# Wanaopiga simu za uongo Zimamoto kuchukuliwa hatua

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mbeya, limesema litawachulia hatua baadhi ya watu wanaopiga simu za dharura na kutoa taarifa za uongo, kuomba fedha na kuwatongoza maofisa wanaopokea simu hiyo.

Limesema tabia hiyo inayofanywa na baadhi ya wananchi wa mkoa huo imekuwa ikichelewa kupokelewa kwa taarifa sahihi za majanga.

Kamanda wa Jeshi hilo Mkoa wa Mbeya, Mrakibu wa Zimamoto, Malumbo Ngata, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mafunzo maalumu ya kukabiliana na majanga kwa waandishi wa habari wa mkoa huo.

Mafunzo hayo yaliandaliwa kwa ushirikiano kati ya jeshi hilo na Chama cha Waandishi wa Habari wa Mkoa wa Mbeya (MBPC) kwa lengo la kuwajengea uwezo wanahabari kuripoti habari za majanga.

Kamanda Ngata alisema wamekuwa wakipokea simu nyingi kila siku ambazo wahusika wanatoa taarifa za uongo kuhusu majanga pamoja na mambo mengine yakiwamo ya kuomba fedha na kuwatongoza maofisa wa jeshi hilo hasa wanawake.

Alisema simu hizo wakati mwingine zimekuwa zikisababisha kuchelewa kupokelewa kwa taarifa sahihi za watu ambao kweli wanakuwa wanahitaji msaada jambo ambalo alisema linahitaji elimu kuendelea kutolewa kwa wananchi.

"Kwa sasa tumeanza kuchukua hatua, tunazichukua namba za wahusika hao na kuzipeleka kwa wenzetu Jeshi la Polisi ili wasakwe na kuchukuliwa hatua za kisheria, wengi wamekuwa wakipiga simu lakini ukipokea unasikia anasema 'nilikuwa najaribu kama inapatikana,' 'naomba hela' na ikitokea askari aliyepokea ni mwanamke anatongozwa," alisema Ngata.

Alisema kwa mwaka 2023 yalitokea majanga 100 ambayo kati yake 80 yalikuwa ya moto na 20 yalikuwa ya uokoaji na kwamba katika matukio hayo kilitokea kifo cha mtu mmoja ambaye alitumbukia kwenye kisima alichokuwa anachimba akakosa hewa.

Mwanaseheria wa Jeshi hilo Mkoa wa Mbeya, Zawadi Maligha, alisema baadhi ya maeneo wamekuwa wakishindwa kukabiliana na majanga ya moto kwa wakati kutokana na mpangilio mbovu wa makazi ya wananchi ambao hauzingatii suala la majanga.

Alisema kuna baadhi ya maeneo katika barabara za mitaa miundombinu yake inakwamisha magari ya jeshi hilo kupita wakati wa kwenda kukabiliana na moto na hivyo kulazimika kuunganisha mipira umbali mrefu.

"Kadiri unavyounganisha mipira hii ya m aji ndivyo hata kasi inapungua, kwahiyo kwenye makazi holela huwa tunapata shida kuzima moto maana tunalazimika kusimamisha gari umbali mrefu," alisema Maligha.

Alisema kwa mujibu wa sheria ya za nchi mtu yeyote anapojenga nyumba lazima apeleke ramani yake kwa jeshi hilo ili ashauriwe vitu vya kuweka kwa ajili ya kukabiliana na majanga mbalimbali yakiwamo ya moto.



Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mkoa wa Mbeya, Mrakibu wa Zimamoto Malumbo Ngata, akitoa elimu ya kukabiliana na majanga ya moto kwa waandishi wa habari wa Mkoa wa Mbeya pamoja wanafunzi wa shule mbalimbali za msingi za mkoa huo mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Rais Samia mgeni rasmi Wiki ya Amani na Maridhiano

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye Maadhimisho ya Wiki ya Amani na Maridhiano nchini ambayo kitaifa yanatarajiwa kufanyika mkoani Mbeya Machi 6, mwaka huu.

Jumuiya ya amani na maridhiano nchini inaundwa na viongozi wa dini na viongozi wa mila na inadaiwa kuwa iliundwa kwa lengo la kuisaidia serikali kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa amani na utulivu kwa taifa.

AKipozungumza na waandishi wa habari na viongozi wa Jumuiya ya Amani na Maridhiano wa wilaya zote za mkoa huo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema maandalizi ya maadhimisho hayo yanaendelea.

Homera alisema kabla ya siku hiyo ya kilele zitakuwa zinafanyika shughuli mbalimbali za kijamii ndani ya mkoa huo ikiwemo uchangiaji wa damu, upandaji wa miti kwenye maeneo mbalimbali kwa ajili ya kutunza mazingira pamoja na michezo mbalimbali.

Alisema mbali na matukio hayo pia viongozi wa jumuiya hiyo wataendesha kampeni maalum ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto katika maeneo yote ya mkoa huo ili kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu vitendo hivyo na namna ya kuvikabili.

"Naomba niwaagize wakuu wa wilaya zote za mkoa huu washirikiane na kamati hizi kutekeleza majukumu haya, kule Kyela tayari uchangiaji damu umeanza na nimepata taarifa kwamba zimeshakusanywa uniti zaidi ya 100 naomba na maeneo mengine muendelee ili tuokoe maisha ya watu wetu," alisema Homera.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano ya Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Oscar Ongere, aliwaomba wadau mbalimbali wa maendeleo mkoani humo kuiunga mkono jumuiya hiyo ili itekeleze vizuri majukumu yake kabla ya siku ya kilele.

Alisema wanakusudia kupanda miti zaidi ya 2,000 katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo kwenye vyanzo vya maji na kwenye maeneo mengine yakiwamo ya taasisi za umma.

Alisema ili kutekeleza majukumu hayo wanahitaji kushirikiwa mkono na wadau mbalimbali kwa maelezo kuwa wanahitaji vitendea kazi kwa ajili ya kutekeleza majukumu hayo.

"Tunawashukuru wenzetu Benki ya CRDB wametupatia miti 2,000 ambayo tutaipanda kwenye maeneo mbalimbali, lakini pia tunawaomba wadau watusaidie kwenye uchangiaji wad amu ili tufikie lengo la kukusanya uniti 1,000," alisema Mchungaji Ongere.

Mwenyekiti wa Machifu wa Wilaya ya Mbeya, Rocket Mwashinga, aliiomba serikali kusimamia vizuri sheria ya mazingira ili kuzuia uharibifu wa mazingira hasa ukataji wa miti ovyo ambao unasababisha mabadiliko ya tabianchi.

Alisema misitu mingi inayosimamiwa na serikali kupitia taasisi zake ndiyo inayoharibiwa tofauti na inayosimamiwa na machifu kwa maelezo kuwa misitu ya machifu hakuna mtu anayeruhusiwa kuingia na kufanya shughuli zake zaidi ya wao wenyewe.

# DC kuwashughulikia madiwani wasio waadilifu

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MKUU wa Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, Jaffar Haniu, amesema hatosita kuwashughulikia baadhi ya madiwani wa wilaya hiyo wanaowashawishi wananchi kuvunja sheria na kuwaahidi kuwa watawalinda endapo watatakiwa kuchukuliwa hatua.

Haniu aliyasema hayo kwenye kikao cha baraza la madiwani wa halmashauri ya wilaya hiyo ambacho kilikuwa na lengo la kupitia rasimu ya bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 ambapo alisema ana taarifa za madiwani hao.

Alisema baadhi ya wajasiriamali wa wilaya hiyo wamekuwa wakifanya biashara kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara ambako hawaruhusiwi kisheria kwa kushawishiwa na madiwani jambo ambalo alisema hawastahili kufanya hivyo.

Alisema madiwani hao wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kuwahamasisha wananchi kufuata sheria badala ya kutumia vibaya madaraka yao.

"Jioni kuna baadhi ya wajasiriamali unakuta wamehama sokoni wamekaa na bidhaa zao pembezoni mwa barabara jambo ambalo ni hatari kwao na hawaruhusiwi, lakini ukifuatilia inasemekana wapo baadhi yenu wanawalinda kwa sababu eti ni wapiga kura tusiwasumbue," alisema Haniu.

Alisema baadhi ya madiwani hao wanawashawishi wananchi kutochangia shughuli za maendeleo kwa madai kuwa jukumu hilo linatekelezwa na serikali pekee hatua inayokwamisha juhudi za maendeleo katika utoaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi.

Alimwagiza mwenyekiti wa halmashauri hiyo azungumze na madiwani ili kuwakumbusha majukumu kulinda usalama wa wananchi na mali zao tofauti na ambavyo wamekuwa wakifanya siku zote.

Aliagiza halmashauri iendeshe operesheni ya kuwaondoa wafanyabiashara waliopo kwenye maeneo yote hatarishi hasa barabarani nyakati za jioni lakini.

Diwani wa Kata ya Msasani, Robin Kapesa aliomba kuboreshwa kwa miundombinu katika maeneo maalumu yaliyotengwa kwa ajili ya wafanyabishara hususani katika soko la Madonde kwa maelezo kuwa eno hilo sio rafiki kwa wafanyabiashara.

Alisema soko hilo kipindi hiki cha mvua halifai kutokana na kujaa matope hali ambayo inasababisha wafanyabiashara kukimbilia kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Mpokigwa Mwankuga, aliahidi kuyafanyia kazi maelekezo ya Mkuu wa Wilaya kwa kuhakikisha madiwani wake wanafuata taratibu zilizowekwa ikiwamo kuhamasisha wananchi kuchangia miradi ya maendeleo.

Vilevile alisema watawahamasisha wananchi kuacha kufanya biashara kwenye maeneo ya hifadhi za Barabara kwa ajili ya usalama wao na kwenda kufanyia shughuli zao kwenye maeneo maalumu.



## Awamu ya pili huduma jumuishi mbioni kuanza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar, inatarajia kuanza awamu ya pili ya zoezi la utoaji wa huduma jumuishi ikiwamo chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi kwa wasichana wote wenye umri wa miaka 14.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, Mkurugenzi Kinga na Elimu ya Afya kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Dk. Salim Salim, alisema huduma hiyo itaanza Desemba mosi hadi mbili, mwaka huu kwa wasichana wote wa Unguja na Pemba.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Afya ilizindua rasmi chanjo dhidi ya ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi Aprili 19, 2018 ili maradhi hayo yasiwe tena tishio kwa wanawake na wasichana.

Alisema zoezi la utoaji wa huduma jumuishi za upimaji wa macho, kuangalia hali ya lishe na utoaji wa chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi kwa awamu ya kwanza lilifanyika Juni, 2023 kwa wasichana wenye umri wa miaka 14 na kufikia wasichana ambapo vigori 100.

Aidha, alisema huduma nyingine jumuishi walipatiwa pia watoto wengine wenye umri wa miaka tisa hadi 14 wakiwamo wavulana.

Alisema ugonjwa huo unaongoza kwa kuathiri wanawake wengi Tanzania na kinamama zaidi ya 7,000 wanagundulika kila mwaka.

Mkurugenzi Salim alibainisha kuwa kinamama kati ya 4,000 hadi 5,000 hufariki kila mwaka Tanzania kutokana na saratani ya mlango wa kizazi huku zaidi ya asilimia 50 wakipoteza maisha.

Alisema saratani ya mlango wa kizazi ina athari kubwa kwa kinamama kote ulimwenguni.

Hata hivyo, alisema inakadiriwa kuwa, wastani wa wanawake 528,000 wanagundulika kuwa na saratani ya mlango wa kizazi kila mwaka na wengi wa wanaoathirika wanatokea katika nchi zinazoendelea ikiwamo Zanzibar na maradhi hayo ni tatizo kubwa la kiafya kwa Zanzibar.

"Hali hii inatishia ustawi wa kinamama wa Zanzibar na iwapo hatua za kukinga na kudhibiti ugonjwa huu hazikuchukuliwa haraka na kwa umakini, kinamama wengi wataendelea kupoteza maisha kila siku kwa sababu ya ugojnwa wa saratani ya mlango wa kizazi ambao unaweza kuzuilika kwa chanjo," alisema.

Akizungumzia njia kubwa tatu za kuthibiti ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi alisema kinga ya awali ni kuhakikisha wasichana wanapata chanjo ya kuwakinga na saratani ya mlango wa kizazi inayojulikana kwa jina la HPV-Human Papilloma Virus Vaccination.

Alisema chanjo ya HPV inasaidia kinga dhidi ya virusi vya HPV vinavyosababisha saratani ya mlango wa kizazi.

Aidha, Mkurugenzi Salim aliwataka vijana kujiepusha na vitendo vya ngono katika umri mdogo, kuepuka uvutaji wa sigara na matumizi ya tumbaku, kuepuka kubeba mimba katika umri mdogo na baadaye kuwa waaminifu katika ndoa kwa vile virusi vya HPV husambaa zaidi kwa njia ya kujamiiana.

# BOT yaanza rasmi kutumia mfumo mpya sera ya fedha

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI Kuu ya Tanzania (BOT), imeanza kutumia mfumo mpya wa uandaaji na utekelezaji wa sera ya fedha ili kuendana na wakati uliopo sasa wa sayansi na teknolojia.

Naibu Gavana wa Sera za Uchumi na Fedha Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Dk. Yamungu Kayandabila, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari katika Ofisi za BOT visiwani Zanzibar.

Alisema taasisi hiyo imeamua kuacha kutumia mfumo wa zamani kutokana na kuwa na ufanisi mdogo wa masuala ya huduma za kifedha kulingana na wakati uliopo hivyo mfumo mpya unalenga kuleta ufanisi katika kutekeleza sera ya fedha nchini Tanzania.

Akitaja majukumu makuu ya benki hiyo Naibu Yamungu, alisema kama zilivyo Benki Kuu zote duniani kazi kuu za BOT ni kusimamia sera ya fedha, kudhibiti mfumuko wa bei na ndio chombo pekee cha kitaifa kilichopewa mamlaka ya kuchapisha fedha za Tanzania na kusimamia taasisi zote za kifedha nchini, ikiwamo benki ili kuhakikisha uchumi endelevu na kulinda haki za wateja wa miamala ya kifedha.

Akizungumzia sera ya fedha na sera ya bajeti, alisema ni shilingi moja yenye pande mbili hivyo ni lazima kupitia katika maeneo yote hayo ili kujenga uelewa jinsi sera mbili zinazofanana.

Akizungunzia sheria za huduma ndogo za fedha uliyopitishwa mwaka 2018 alisema BOT imepewa jukumu la kusimamia hilo kwa kuona inaanzisha sera ili kuendelea kusimamia jambo hilo kwa kushirikiana na serikali.

Hata hivyo, alisema tayari BOT imeanzisha idara inayosimamia malalamiko ya wateja wa fedha ambapo hapo nyuma hakukuwa na idara hiyo jambo ambalo ni mageuzi makubwa ndani ya BOT hivyo aliwataka wananchi kutumia idara hiyo kuwasilisha malalamiko yao ili kushughulikiwa kwa haraka.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Benki Kuu ya Tanzania tawi la Zanzibar, Masoud Suleiman, alisema lengo la mafunzo hayo ni kupata uelewa wa kazi wanazozifanya benki.

Akiwasilisha mada ya utekelezaji wa sera ya fedha Meneja Msaidizi Uchambuzi wa Sera ya Fedha, John Mero, alisema mafanikio ya kiuchumi yanategemea sera mbalimbali ikiwamo sera ya fedha, sera za kibajeti na sera ya kisekta ambazo zitasaidia kufia malengo ya nchi.

Aidha alisema sera ya fedha hujumuisha uamuzi na hatua zinachukuliwa na BOT kupunguza, kuongeza ujazo wa fedha ili kufikia malengo ya kiuchumi. Alisema malengo ya sera hiyo ni kuhakikisha kiwango cha fedha kilichokuwapo kwenye uchumi kinakidhi mahitaji kwa kuwa kiwango kikubwa cha fedha katika mzunguko zaidi ya mahitaji ya shughuli za uchumi hupelekea kuongezeka kwa bei za bidhaa.

Meneja Msaidizi Utafiti BOT, Lusajo Mwamkemwa, alisema malengo ya sera ya fedha ni kudhibiti mfumuko wa bei, kuvutia uwekezaji, uzalishaji, biashara, kulinda uwezo wa wananchi kumudu gharama za maisha.



Meneja wa Kampuni ya Jumaco Property LTD inayojihusisha na utoaji wa misaada mbalimbali ya kijamii isiyojiweza na upimaji na uuzaji wa viwanja Dodoma, Sabinus Mathew (kulia), akizungumza na watoto yatima pamoja wafanyakazi wa Kituo cha Shirika la Mtakatifu Ursulu Miyuji nyumba ya matumaini, Dodoma baada ya kukabidhi misaada mbalimbali jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wizara yaingilia kati mgogoro wa ardhi Ndunduke

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Rahma Kassim Ali, amesema wizara itaupatia ufumbuzi mgogoro wa ardhi uliodumu kwa muda mrefu kwa wananchi wa Ndunduke ili wananchi waendelee na shughuli zao.

Waziri Rahma aliyasema hayo jana wakati alipofika katika eneo hilo lililopo Dole Wilaya ya Magharibi "A" Mkoa wa Mjini Mgaharibi Unguja.

Waziri huyo aliziagiza pande zote zilizomo katika mgogoro huo kutotumia nguvu na serikali italipatia ufumbuzi suala hilo ndani ya muda mfupi na kila mmoja atapata haki yake.

Aidha, Waziri Rahma ameiagiza kamisheni ya ardhi baada ya mgogoro huo kupatiwa ufumbuzi kulipima eneo hilo sambamba na kufanya utambuzi mara moja.

Aidha amewasisitiza wananchi hao kuendelea kutii agizo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya la kutoendelea na ujenzi wowote katika eneo hilo wakati serikali ikiupatia ufumbuzi mgogoro huo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Magharibi "A", Suzan Peter Kunambi, ameushukuru uongozi wa wizara hiyo kwa hatua iliyoanza kuzichukua baada ya mgogoro huo kufikishwa katika Ofisi ya Waziri.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mzee Haji Ali, alisema wizara itaenda kuunda timu ya watu kumi itakayoshirikisha pande zote na kuanza kukaa vikao vyake ili kuipatia ufumbuzi changamoto hiyo.

# Ubovu wa barabara washtua, halmashauri yatenga bajeti

**Na Julieth Mkireri, CHALINZE**

BARABARA nyingi za vijijini zimekuwa vikwazo kwa wananchi kuendesha shughuli zao hususani za usafirishaji katika kipindi cha mvua, huku baadhi ya wanafunzi wakikwama kwenda shuleni.

Mvua iliyonyesha hivi karibuni iliweka wazi ubovu wa barabara kwenye maeneo mengi na kusimamisha mipango ilivyokuwa itekelezeke kwa kipindi hicho.

Katika kukabiliana na hali hiyo mwaka wa fedha ujao 2024/25, Halmashauri ya Chalinze, mkoani Pwani imetenga kuhamisha Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya kuwezesha Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) kuboresha barabara za vijijini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chalinze, Ramadhani Possi, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao maalum cha Baraza la Madiwani.

Alisema kuwa kulingana na maelekezo ya mwongozo, fedha hizo kwa TARURA zitafanya kazi ya kuweka taa, ununuzi wa greda na uchongaji barabara.

Baraza la Madiwani lilipitisha Makisio ya Mpango wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25 Sh. bilioni 54.5, mapato ya ndani yakiwa ni Sh. bilioni 17.3, ruzuku kutoka Serikali Kuu na matumizi ya kawaida zaidi ya Sh. bilioni 26 na miradi ya maendeleo Sh. bilioni 11.2 ambapo Serikali Kuu ni Sh. bilioni 6.3 na wahisani Sh. bilioni 4.9.

Akiwasilisha taarifa ya makisio hayo kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Ofisa Mipango wa Halmashauri hiyo, Ismail Bilali alisema bajeti hiyo ni ongezeko la asilimia 4.07 kulinganisha na bajeti ya mwaka 2023/24 ambayo ilikuwa Sh. bilioni 52.5.

Bilali alisema katika bajeti hiyo, matumizi ya mapato ya ndani yameelekezwa zaidi katika kutatua vikwazo vilivyojitokeza katika mwaka ambao wanatekeleza bajeti yake.

Akizungumza baada ya kuwasilishwa kwa bajeti hiyo, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Hassan Mwinyikondo alisema madiwani watashirikiana na watumishi katika utekelezaji bajeti hiyo hususani kwenye kusimamia miradi ya maendeleo.

Diwani wa Kiwangwa, Malota Kwaga alisema Idara ya Ustawi wa Jamii katika halmashauri hiyo haifanyi kazi kama inavyotakiwa katika mapambano dhidi ya ukatili kwenye kata, hivyo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chalinze anapaswa kufanyia kazi suala hilo.



Wahitimu 40 wa vyuo mbalimbali nchini ambao wanatarajia kuanza mpango wa mafunzo kazini kwa vitendo unaodhaminiwa na kampuni ya GGML kwa mwaka 2024/25 wakiwa pamoja baada ya kukaribishwa rasmi mwishoni mwa wiki mkoani Geita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi 40 kunufaika mafunzo vitendo mgodini

**Na Mwandishi Wetu, GEITA**

KATIKA kudhihirisha dhamira ya kujenga wahitimu wa vyuo kukubalika kwenye soko la ajira, Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imezindua mafunzo tarajali kwa wanafunzi 40 waliohitimu vyuo mbalimbali nchini.

Mafunzo hayo yanayotolewa kwa muda wa mwaka mmoja (2024/25), yatahusisha programu mbalimbali ikiwamo za uanagenzi, mafundi mchundo na wataalamu wa masuala ya madini ya fani nyingine ambazo zimeanzishwa ili kukuza ujuzi wa vijana wa kitanzania.

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika mwishoni mwa wiki mkoani Geita, Makamu wa Rais Mwandamizi - Kitengo cha Biashara Afrika, Terry Strong, alisema mpango wa mafunzo hayo huwapa wahitimu wasio na ajira nafasi ya kupata uzoefu wa kazi ambao unakamilisha masomo yao na unaweza kuwasaidia kushindana katika soko la ajira.

Akiwakaribisha wanafunzi hao 40 waliofaulu usaili ili kuanza rasmi mafunzo hayo chini ya udhamini kamili wa GGML, Terry alisema mpango huo ulioanza kutekelezwa mwaka 2009, umenufaisha jumla ya wahitimu 258 (pamoja na waliopo sasa) kutoka vyuo mbalimbali vya elimu ya juu nchini.

Terry pia aliwakaribisha wahitimu 10 wa mafunzo hayo kwa mwaka jana ambao wamepatiwa ajira za kudumu ndani ya GGML.

"Walengwa ni asilimia 41 ya wanawake na asilimia 59 ya wahitimu wa kiume. Kati ya wahitimu 258 walioandikishwa, asilimia 34 (87) waliajiriwa na GGML kwa mkataba wa kudumu katika nafasi mbalimbali ndani ya kampuni, huku wengine wakiajiriwa kwa mkataba wa muda.

"Kwa kuzingatia mafanikio kadhaa yaliyofikiwa hadi sasa, GGML imejitolea kuendelea na mpango wa mafunzo kazini kama mpango muhimu wa kuajiri," alisema.

Alibainisha kuwa mpango huo umetumika kama chanzo kikuu cha wahitimu kuing'arisha GGML kwa vipaji walivyojaliwa na kuwatayarisha kutekeleza majukumu muhimu ndani ya kampuni kwa muda mfupi, wa kati na mrefu na kutoa mfano kuwa waliomaliza mwaka jana, 10 wamepatiwa ajira za kudumu ndani ya GGML. Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela, mbali na kushukuru GGML kwa kutekeleza mpango huo, pia alipongeza kundi hilo la wahitimu wa vyuo mbalimbali wanaobahatika kupata mafunzo GGML kwa mwaka huu 2024/25.

"Kitendo cha kupata fursa hii ndani ya GGML, si njia tu ya kupata uzoefu, lakini ni chachu ya kutambua uwezo wako kwa ukamilifu. Kukabiliana na changamoto, tumia maarifa yako na uruhusu shauku yako ikupeleke kwenye ubora," alisema.

Mkuu wa Idara ya Mafunzo na Ujuzi, Albert Rukeisa, akizungumza katika uzinduzi huo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Chama cha Waajiri (ATE), Suzanne Ndomba - Doran, aliipongeza GGML kwa jitihada zake ambazo kwa zaidi ya miaka 15 zimekuwa chachu kwa waajiri wengine kuendelea kutoa nafasi kwa vijana kujifunza na kuongeza wataalamu wa madini katika sekta hiyo.

Pia alipongeza wanafunzi hao walipata fursa ya kujiunga na mafunzo hayo kwa vitendo kwa mwaka 2024/25.

"Sanjari na hilo nipende kutoa rai kwa vijana hawa, waswahili wanasema "Ukishikwa shikamana". Nendeni mkaweke bidii ya kazi, uaminifu, mkizingatia usalama na taratibu zote za mgodi, nanyi mtayaona mema ya utii na bidii katika kujifunza kazi," alisema.

Mmoja wa wanafunzi waliohitimu mafunzo hayo mwaka jana na kuajiriwa ndani ya GGML, Diana Laswai, mbali na kushukuru GGML, pia alishukuru Serikali kwa kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kutoa mafunzo kazini kwa vitendo.

Pia alitoa wito kwa wanafunzi wapya wanaoanza mafunzo hayo mwaka huu, kufanya kazi kwa bidii, kuzingatia nidhamu na kuzingatia tunu ya GGML ambayo ni usalama.

Grace Msafiri, mmoja wa wanafunzi waliopata fursa ya mafunzo hayo kwa mwaka huu, pia alishukuru GGML kwa kuwapatia fursa na kuwawekea mazingira rafiki ya kazi.

Aliahidi kutumia mafunzo hayo kwa kufanya kazi kwa bidii ili wafike mbali ili na wao wapate fursa za kuajiriwa katika maeneo mbalimbali pindi watakapohitimu.

## Jeshi laita wadau kupitia mitaala mipya ya mafunzo Magereza

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

JESHI la Magereza nchini limekutanisha wadau mbalimbali ili kupitia na kutoa maoni yao kwenye mitaala yake mipya ya mafunzo.

Limesema mitaala hiyo ikianza rasmi kutumika, itawezesha vyuo vyake kuzalisha wataalamu wenye ujuzi wa kutoa mafunzo maalum kwa wafungwa ili wawe raia wema na wazalishaji mali wazuri pindi wakitoka gerezani.

Akizungumza mjini Morogoro mwishoni mwa wiki, Mratibu wa Mtaala wa Mafunzo kutoka Jeshi la Magereza, Dk. Marius Rutta, alisema lengo la kukutanisha wadau hao ni kuhakikisha utekelezaji wa mitaala hiyo unakuwa wa ukamilifu. Mafunzo kwa kutumia mitaala hiyo yanatarajiwa kuanza mwaka huu (2024/25) kwa askari na Watanzania.

Dk. Rutta alisema matatizo ya mabadiliko ya tabia ni ya watu wote walioko gerezani na wale waliomaliza vifungo na kurudi kwenye jamii, hivyo uhuishaji mitaala ya Jeshi la Magereza ni muhimu kwa watu wote.

Mwakilishi wa Chuo Kikuu cha Jordan, Prof. Paul Domick, alisema ni vyema wafungwa wafundishwe namna bora za kujikita katika uzalishaji mali ili kupata kipato pale wanapomaliza kifungo.

"Jukumu la msingi la Jeshi la Magereza ni kupokea na kuhifadhi gerezani watu wote wanaoletwa kwa mujibu wa sheria za nchi na kuendesha programu mbalimbali zenye kulenga kurekebisha wafungwa waliohukumiwa ili hatimaye watoke gerezani wakiwa raia wema," alisema Prof. Domick.

Alisema kuwa katika kutekeleza majukumu hayo, Jeshi la Magereza lina wajibu wa kufuata na kuheshimu sheria zote za nchi pamoja na sheria mbalimbali za kimataifa zinazohusu haki za binadamu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Mafunzo ya Taaluma ya Urekebishaji Tanzania (TCTA), Dk. Zena Mabeyo, alisema mitaala ya upatikanaji wataalamu nao umefikia wakati wake wa kufanyiwa marekebisho ili vyuo vya magereza viweze kuzalisha wataalamu wenye ujuzi wa kutoa mafunzo maalum kwa wafungwa.

Katika kuhakikisha hilo linatimia, Jeshi la Magereza nchini linachukua jukumu la kukutanisha wadau wa jeshi hilo ili kuwapa nafasi ya kutoa maoni yao na kupitia mitaala mipya ya utoaji mafunzo kwa Jeshi la Magereza.

Akifungua kikao hicho kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu kutoka wizara hiyo, Mariam Mmbaga, aliwataka waandaaji wa mitaala hiyo kuhakikisha inakuwa bora ili kusaidia kupatikana kwa maofisa magereza bora ili walete tija na mabadiliko ndani ya jeshi hilo.

Alisisitiza uandaaji wa mitaala unahitaji uzalendo na umahiri na kusisitiza mpaka kufika Septemba mwaka huu, wawe wamekamilika kwa ufasaha.

# Wapalestina wanapokosa pakukimbilia

- Wagoma kuondoka Rafah, vifo vyafikia 28,858



Kiongozi wa kundi la Hamas, Ismail Haniyeh. **PICHA: MTANDAO**

TAKRIBAN Wapalestina milioni 1.5, wengi wao wakiwa wanawake na wototo wameyahama makazi yao na kubanwa katika mji mdogo wa Rafah ulioko kusini mwa Ukanda wa Gaza, eneo ambalo wanadai pia kufukuzwa licha ya wengi kugoma kuondoka wakidai kwamba hawana pa kwenda.

Inaelezwa kuwa wamekuwa wakifukuzwa kutoka kwenye makazi yao katika maeneo mengine ya Gaza wakati wa shambulio la Israel kwenye eneo lililozingirwa, ambalo limeua zaidi ya watu 28,858.

Aidha, eneo la Rafah ambalo Israel ililiteuwa kama sehemu salama kwa wakazi wa Palestina kukimbilia, inaelezwa kuwa kwa sasa jeshi hilo linatishia kuendeleza uvamizi wa ardhini, jambo linalosababisha watu zaidi ya milioni moja kukwama wakiwa na hofu kubwa bila kujua pengine pa kwenda.

Inabainishwa kuwa Rafah ni moja ya maeneo ya yaliyoteuliwa hivi karibuni ambayo Israel inasema yatakuwa maeneo salama kwa watu kujikinga kutokana na mashambulizi ambayo sasa ni miezi minne, lakini Israel imeshambulia moja baada ya jingine na kuwalazimisha watu kutoka nje tena na tena.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, anasema amedhamiria kuendelea na vita, akidai kwamba ataimaliza Hamas, ambayo ndiyo dhamira iliyotangazwa nyuma ya shambulio la Gaza.

Viongozi wakuu wa Hamas wanasema kuwa hatua hiyo kwa upande wa Israel itamaliza uwezekano wowote wa mazungumzo kati ya pande hizo mbili.

Kutokana na hali hiyo, hofu ambayo imewakumba watu huko Rafah inaendelea kujengeka.

**HAWANA PAKUKIMBILIA**

Umm al-Abed Fayyad, anaieleza kwamba yeye na familia yake wameyakimbia makazi yao mara nne hadi sasa.

"Tuko katika eneo tofauti kila mwezi. Mahali pa mwisho tulikuwa Khan Younis, na sasa tuko Rafah," amesema.

**"Tulikuja Rafah, na sasa wanatuambia tuondoke. Kutakuwa na mauaji. Hakuna mahali pengine pa kwenda. Rafah ndio kimbilio letu la mwisho. Mtu yeyote anayehama anauawa. Hatuna mahali salama pa kwenda.Vita hivi lazima vikome," amesisitiza.**

Anapoulizwa kuwa anahisi vipi kuhusu uwezekano wa uvamizi wa Israel, Umm al-Abed Fayyad anasema hana mahali pengine pa kwenda.

"Waisrael wako kila mahali. Tutaenda wapi. Watu wengi wananjaa na hawana makazi. Hata watishe kiasi gani, hatutahama tena, na Mungu akipenda, tutashinda. Tutavumilia na kubaki wavumilivu," amesema.

Asaad Hassan, Mpalestina mwingine aliyefukuzwa kutoka mji wa Gaza hadi Rafah, anasema hayuko sawa na nia yake ni kurejea nyumbani kwake na huku akisisitiza kuwa uvamizi wa Israel ukome.

"Hatuna mahali pengine pa kwenda isipokuwa kaburini, ikiwa watatekeleza vitisho vyao vya kuendelea kuivamia Rafah," amesema.

Vita vya Israel dhidi ya Ukanda wa Gaza uliozingirwa vilianza Oktoba saba, 2023. Baada ya Hamas iliyotawala Gaza, kuanzisha mashambulizi kusini mwa Israel, na kuua watu 1,139 na kurudisha takriban mateka 240 huko Gaza.

Israel ilijibu mara moja kwa mashambulizi ya mabomu na kufuatiwa na uvamizi wa ardhi kaskazini mwa Gaza.

Inaelezwa kuwa takriban Wapalestina 28,858 waliouawa huko Gaza, wengi wao wakiwa wanawake na watoto, huku 67,984 wakiwa wamejeruhiwa katika kipindi cha miezi minne iliyopita.

Kutokana na mashambulizi hayo zaidi ya wakazi milioni 2.3 wa Gaza wamelazimika kutoka nje ya makazi yao na zaidi ya asilimia 60 ya miundombinu yote katika ukanda huo imebomolewa.

Mpalestina mwingine Abu Salme, anasema alihama na familia yake kwenda Rafah kutokana na amri iliyotoka kwa Jeshi la Israeli kwamba eneo hilo litakuwa salama jambo ambalo limekuwa kinyume na matamshi yao.

"Tulikuja Rafah, na sasa wanatuambia tuondoke. Kutakuwa na mauaji. Hakuna mahali pengine pa kwenda. Rafah ndio kimbilio letu la mwisho. Mtu yeyote anayehama anauawa. Hatuna mahali salama pa kwenda.Vita hivi lazima vikome," amesisitiza.

Mohammed Madi, ambaye ni daktari, aliyefukuzwa mara kadhaa tangu alipolazimishwa kuondoka nyumbani kwake katika Jiji la Gaza anasema hataondoka Rafah kwa kuwa hana pahali pa kwenda, akieleza kuwa sehemu iliyobaki ya Gaza inaharibiwa.

"Nitakufa hapa kabla sijaondoka. Tunatoa wito kwa nchi za Kiarabu ... kuchukua uamuzi na kumaliza vita hivi vya mauaji ya halaiki dhidi ya Gaza," amesema.

Wakati hayo yakiendelea Desemba 29, 2023 Afrika Kusini ilifungua kesi dhidi ya Israel katika Mahakama ya Kimataifa ya Haki, ikisema kuwa inatekeleza mauaji ya kimbari dhidi ya watu wa Palestina, eneo ambalo wengi wamelitumia kuelezea vita vya Israel dhidi ya Gaza.

Mwandishi wa habari, Alaa Salameh, mkazi wa Rafah ambaye ameangazia vita kote ukanda huo, anasema ataendelea kuripoti kutoka katika jiji hilo licha ya vitisho vya Israel.

"Uvamizi wa Israel huko Gaza haufuati sheria za kimataifa. Hakuna sehemu salama. Kuna haja ya kuwa na shinikizo la kimataifa ili kuzuia uhalifu huu unaowezekana kutokea," amesema.

Anabainisha kuwa Israel tayari imeua maelfu ya Wapalestina katika mashambulizi ya anga katika mji wa Rafah katika siku chache zilizopita.

Haifaa Saleh, anaeleza kuwa alilazimika kuondoka nyumbani kwake katika Jiji la Gaza na kwenda Rafah "Tuliondoka Oktoba 14. Hatukutaka kuondoka katika Jiji la Gaza au katika nyumba zetu, lakini uvamizi wa Israel ulituambia kwamba tungekuwa salama ikiwa tutafanya hivyo. Na waliteketeza kila kitu huko Gaza".

**HAMAS**

Wakati hayo yakiendelea kiongozi wa kundi la Hamas, Ismail Haniyeh, amesisitiza masharti ya kundi hilo ya usitishaji kamili wa vita huko Gaza.

Msimamo huo umetangazwa siku moja baada ya Rais wa Marekani, Joe Biden, kutoa wito wa kusitishwa vita kwa muda ili kutoa fursa ya kuachiwa huru kwa mateka na wafungwa.

Inaelezwa kuwa mazungumzo ya ngazi ya juu ya kusimamisha vita vya Israel na Hamas yalifanyika siku chache zilizopita mjini Cairo, Misri, lakini matokeo yake bado hayajawa wazi.

Haniyeh anayeishi nchini Qatar, anasema kundi hilo halitokubaliana na chochote kilicho chini ya usitishaji vita, kuondolewa kwa vikosi vya jeshi la Israel kutoka Gaza, kuondoa mzingira na kutoa hifadhi salama kwa watu walioyahama makazi yao.

Rais Biden ametoa wito wa usitishaji wa muda wa mapigano Gaza ili kuachiwa mateka kwa uwezekano wa kubadilishana wafungwa wa Kipalestina wanaoshikiwa Israel.

Familia za mateka wa Israel zimezidisha shinikizo dhidi ya Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu, kumtaka afikie mwafaka wa kuwezesha kuachiwa kwao.

# NAHODHA KMC AELEZA SABABU KUTWANGWA MAKONDE UWANJANI

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa KMC, Awesu Awesu, ameeleza sababu ya wachezaji wawili wa timu yake, kipa Wilbol Maseke na Ibrahim Elias, kutwangana makonde katika mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Yanga juzi, Uwanja wa Jamhuri, Morogoro, akidai kuwa ni vijana na damu zilikuwa zinachemka, huku kila mmoja akiwa anaonekana hataki kufungwa.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Awesu amekiri kuwa halikuwa tukio zuri, lakini akafafanua kuwa kwenye dunia ya soka vitu hivyo vipo hata kwenye ligi mbalimbali barani Ulaya na kwingine hutokea.

Katika mechi hiyo, kipa Maseke mara kwa mara alionekana kuwafokea mabeki wake ambao walionekana kufanya uzembe anapowaanzishia mipira, lakini nao pia walikuwa wakimlalamikia, kitu ambacho kilishia kwa tukio hilo.

Baada ya tukio hilo, Maseke hakurejea tena uwanjani dakika 45 za pili, nafasi yake ikichukuliwa na Denis Richard ambaye alipachikwa mabao mawili kati ya matatu ambayo KMC ilipoteza dhidi ya Yanga.

"Wachezaji wetu wana nidhamu, nadhani hili ni tukio la kwanza msimu huu, na katika mechi kama hii kubwa hakuna mchezaji anayetaka kufungwa, haiwezekani mkaambizana taratibu kukaba ni lazima mtaambiwa kwa sauti kubwa, kali na yenye msisitizo, lakini anayeambiwa damu yake imechemka, lazima vitu kama hivi wakati mwingine vinatokea, nadhani siyo Tanzania tu, hata kwa wenzetu. Naamini hakiwezi kutokea tena, kila mchezaji tutakaa naye chini na kulizungumza hili liishe," alisema nahodha huyo.

Katika mechi hiyo ambayo Yanga ilishinda mabao 3-0, wachezaji wa KMC walionekana kupasiana pasi nyingi ndani ya eneo la hatari, huku wakimrudishia kipa wao mipira bila umakini wowote, kitu ambacho kilisababisha wakoswekoswe mara kwa mara, kwani wapinzani wao walikuwa wakichukua mipira na kusababisha madhara makubwa, na ilikuwa bahati tu kufungwa idadi hiyo ya mabao.

Clement Mzize peke yake alikosa mabao manne ya wazi, Pacome Zouzoua na Maxi Nzengeli walikosa mara moja kila mmoja, Kennedy Musonda mara mbili na Joseph Guede mara mbili pia.




Mshindi wa Mchongo Jackpot ya Sh. milioni 250 kupitia Betway, Peter (katikati), akifurahia baada ya kukabidhiwa mfano wa hundi mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Ruvuma yatoa tena mshindi Jackpot mil. 250/- za Betway

**Na Mwandishi Wetu**

KWA mara nyingine tena Mkoa wa Ruvuma umetoa mshindi wa Mchongo Jackpot ya Sh. milioni 250 kupitia Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya Betway Tanzania, hii ikiwa ni baada ya awali Bernard M, aliyejinyakulia ushindi huo Desemba mwaka jana, wakati huu ni Peter L, kutoka Wilaya ya Mbinga mkoani humo.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhiwa hundi yake katika hafla iliyofanyika katika Ofisi za Betway Tanzania jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki Peter, alisema imekuwa kama ndoto kupata kiasi hicho cha fedha kwenye siku yake ya kuzaliwa.

Anasema hakutegemea hata siku moja kama angeweza kushindi na kuingia katika kundi la matajiri nchini huku akiwasisitiza wananchi wengine kushiriki katika kubashiri na michezo mingine inayoendeshwa kupitia Betway Tanzania.

Aidha, ameushukuru uongozi mzima wa Betway Tanzania kwa ushirikiano waliuonyesha tangu alipotangazwa kuwa mshindi hadi hatua ya kukabidhiwa fedha zake huku akisisitiza kuwa ataendelea kubashiri zaidi na zaidi kupitia kampuni hiyo kwa kuwa inaaminika.

Kwa upande wa Meneja Masoko wa Betway Tanzania, Calvin Mhina, mbali na kumpongeza mshindi huyo alisema kampuni hiyo imekuwa karibu na wateja wake wakati wote huku akisisitiza kuwa ushindi na malipo kwa mshindi huyo ni kielelezo cha uaminifu wa kampuni hiyo.

Alisema wao kama kampuni bora ya michezo ya kubashiri Tanzania na duniani kote ushindi huo unawafanya kuendelea kujiweka mbele zaidi hasa kwa kuwa na promosheni nyingi nzuri zinazomwezesha mtu kushinda kwa urahisi.

## Washindi DAM DAM Marathon 2024, wazawadiwa fedha

**Na Sabato Kasika**

WASHINDI 18 wa mbio za 'DAM DAM' Marathon 2024 zilizoshirikisha wakimbiaji zaidi ya 2,000, wamejinyakulia kitita cha Sh. milioni 7. 8.

Mbio hizo za kilomita tano, 10 hadi 21 (nusu marathon), zilianzia katika viwanja vya Leaders Club jijini Dar es Salaam jana, kuelekea Agakhan hadi Masaki Mwisho na kuishia viwanjani hapo.

Washindi wa kwanza wa kilomita 21, walikuwa ni Herman Sulle na Fabian Nelson ambao walijinyakulia kitita cha Sh. milioni mbili, huku Jonas John na Paul Festo walioshika nafasi ya pili wakiondoka na Sh. milioni 1.5.

Dickson Paul na Aloyce Sambu walikuwa washika nafasi ya tatu na kujishindia Sh. milioni moja.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya utoaji wa zawadi hizo, Ofisa Uhusiano wa Clouds, Dotto Bahemu, alisema washindi wa kwanza wa mbio za kilomita 10 walikuwa ni Jamal Said na Shomary Mohamed ambao walipata kitita cha Sh. milioni moja.

"Mbio za DAM DAM Marathon' 2024 zilihusisha watu wawili wawili, mtu na rafiki yake, mpenzi wake au mkewe waliokimbia pamoja," alisema Bahemu.

Alitaja washindi wa pili wa mbio hizo kuwa ni John Joseph na Ribertino Robert waliozawadiwa Sh. 800,000, huku washindi wa tatu wakiwa ni Alfred Sulle na Modest Petro ambao walizawadiwa Sh. 500,000.

"Washindi wa kwanza wa mbio za kilomita tano ni Elibariki Buko na Emmanuel Josephat walioondoka na Sh. 500,000.

"Kwa upande wa washindi wa pili ni Gerald Salum na Samuel Nyangora, ambao walizadiwa Sh. 300,000, huku washindi wa tatu wa mbio hizo wakiwa ni Mathayo Jeremiah na Paul Masenza waliopewa kitita cha Sh. 200,000," alisema.

Bahemu alifafanua; "Tunawashukuru wadau wakiwamo Jeshi la Polisi kwa kusimamia usalama maeneo yote ambayo wakimbiaji walipita, pia DSTV, Faras, Afya Maji kwa jinsi walivyofanikisha mbio hizo."

## ZISIKUPITE

### MBAPPE NAMBA 10
REAL Madrid wamebakiza jezi namba 10 kwa Kylian Mbappe iwapo atajiunga nao akitokea Paris St-Germain msimu huu wa joto. **(Mundo Deportivo)**

### KUTUA MWISHO WA MSIMU
RAIS wa Klabu ya Real Madrid, Florentino Perez, amewaambia wachezaji wa Real Madrid kwamba Kylia Mbappe atajiunga na timu hiyo ya Hispania mwishoni mwa msimu huu. **(Footmercato)**

### MILAN KUMUUZA LEAO
AC Milan itazingatia ofa zaidi ya euro milioni 100 kwa mshambuliaji wa Ureno, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 24, ambaye pia amehusishwa na Paris St-Germain kama mbadala wa Kylian Mbappe. **(Gazzetta dello Sport)**

### CITY KUMBAKISHA HAALAND
KLABU ya Manchester City ina imani kuwa Real Madrid ikimsajili Kylian Mbappe itakuwa na nafasi nzuri ya kumshawishi mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 23 kusaini mkataba mpya hadi 2029. **(Mirror)**

### CHELSEA NA OSIMHEN
CHELSEA ipo tayari kuzingatia kipengele cha kutolewa cha pauni milioni 111 ili kumsajili mshambuliaji wa Napoli mwenye umri wa miaka 25, Victor Osimhen. **(Rudy Galetti)**

### TEL AVUTIA
MANCHESTER United inavutiwa na mshambuliaji wa Bayern Munich mwenye umri chini ya miaka 21 wa Bayern Munich. Mathys Tel. **(Sky Sports)**

### ROWE AWINDWA
KLABU za Newcastle na Aston Villa zinaongoza mbio za kumnunua kiungo mshambuliaji wa Arsenal, Emile Smith Rowe mwenye umri wa miaka 23. **(Football Insider)**

### ASHWORTH AMTAKA MACAULAY
MKURUGENZI wa Michezo wa Newcastle United, Dan Ashworth, ambaye amefuatwa na Manchester United atajaribu kumleta mchambuzi mkuu wa Chelsea, Kyle Macaulay ikiwa atahamia Old Trafford. **(Sun)**

### GLASNER KESHO PALACE
KOCHA Oliver Glasner atafanya mazoezi yake ya kwanza na Crystal Palace Jumanne baada ya kuteuliwa kwake kama mrithi wa Roy Hodgson kuthibitishwa. **(Fabrizio Romano)**

### TEDEN LULU LEVERKUSEN
KLABU ya Bayer Leverkusen imekuwa ikimsaka beki wa Luton mwenye umri wa miaka 21, Teden Mengi. **(Mirror)**

### BAYINDIR AFIKIRIWA
KLABU ya Galatasaray inafikiria kumnunua mlinda mlango wa Manchester United mwenye umri wa miaka 25 kutoka Uturuki, Altay Bayindir, ambaye amecheza mechi moja tu tangu ajiunge nayo akitokea Fenerbahce msimu uliopita wa majira ya joto. **(Sport)**

### STEIDTEN KUBAKISHWA
WEST Ham ina imani kuwa inaweza kumbakiza Mkurugenzi wa Ufundi, Tim Steidten, licha ya kutakiwa Liverpool. **(Mirror)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RASHFORD AMULIKWA PSG KUWA MRITHI WA MBAPPE

Katika orodha hiyo, yumo pia mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen ambaye...

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya PSG imeripotiwa kumtaja Marcus Rashford katika orodha fupi ya wachezaji wanaotarajiwa kuchukua nafasi ya Kylian Mbappe.

Kwa muda mrefu Mbappe amekuwa akihusishwa na kutaka kuondoka hapo Parc des Princes, huku Real Madrid ikitajwa kuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kumsajili nyota huyo wa Kimataifa wa Ufaransa.

Sakata la muda mrefu kuhusu mustakabali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, lilichukua mkondo wake wiki hii, huku Mbappe akiitaarifu klabu hiyo kwamba ataondoka bila malipo mkataba wake utakapokamilika msimu wa majira ya joto.

Kwa mujibu wa ripoti kupitia gazeti la The Times, mshauri wa soka wa klabu hiyo ya Paris, Luis Campos, anamuona Rashford kama mbadala sahihi wa Mbappe.

Rashford alikuwa kwenye mazungumzo ya kujiunga na klabu hiyo ya Ligue 1 msimu wa majira ya joto wa 2022 kabla ya kubaki United na kufurahia kampeni yake nzuri zaidi kufikia sasa Old Trafford, akifunga mabao 30 katika mechi 56 kwenye michuano yote.

Hata hivyo, amekuwa na wakati mgumu wa kuendeleza kiwango chake cha juu katika msimu wa pili wa Erik ten Hag kuinoa klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ana mabao matano pekee ya Ligi Kuu England katika mechi 23 alizocheza msimu huu, huku kutocheza vizuri uwanjani kukiwa na matukio ya kutatanisha nje ya soka.

Januari mhitimu huyo wa akademi alikosa mazoezi kabla ya mechi ya Kombe la FA dhidi ya Newport baada ya kupigwa picha katika klabu ya usiku ya Belfast, na tukio hilo liliripotiwa kuwa na utata kwenye chumba cha kubadilishia nguo cha klabu hiyo.

Majira ya joto yaliyopita Rashford alisaini mkataba mpya wa miaka mitano Old Trafford wenye thamani ya kulipwa mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki.

Kwa hiyo, mshambuliaji huyo anaweza kuamuru ada kubwa, huku Sir Jim Ratcliffe akiwa na sauti ya mwisho juu ya uwezekano wowote wa kuondoka.

Rashford amejumuishwa kwenye orodha ya wanaotamaniwa na PSG na mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen.

Osimhen amekuwa muhimu kwa Klabu ya Napoli tangu awasili klabuni hapo akitokea Lille mwaka 2020.

Osimhen alikuwa mfungaji bora wa klabu hiyo huku Luciano Spalletti akiwaongoza kutwaa taji la kwanza la Serie A baada ya zaidi ya miongo mitatu msimu uliopita.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria alizawadiwa kwa kiwango kizuri zaidi kwa kuongezewa mkataba Desemba, huku kipengele cha kutolewa kiliripotiwa kuwa zaidi ya pauni milioni 105.

Chelsea na Arsenal pia wanaripotiwa kutaka kumsajili Osimhen msimu wa majira ya joto, lakini mshambuliaji huyo hivi majuzi alisisitiza kwamba tayari ameshaweka ramani ya maisha yake ya soka.

„Kuna uvumi kuhusu mimi kuhusishwa na Ligi Kuu England,“ alisema Osimhen akiiambia CBS Sports mwezi uliopita.

“Unapokuwa mmoja wa washambuliaji moto zaidi duniani, unatarajia jambo la aina hii.

“Bila shaka, EPL ni mojawapo ya ligi kubwa na bora zaidi duniani kote.

„Nikiwa Napoli, ndiyo kwanza nimetia saini mkataba mpya, ninafurahia muda wangu huko.”

“Ninajua ninachotaka kufanya. Tangu nianze nimekuwa mtu wa kuchukua maamuzi yangu na kila kitu kinaniendea japo nilipoanza hakikwenda sawa na nilichopanga, lakini tayari nilikuwa na mpango wangu. Tayari nilijua hatua inayofuata ninayotaka kuchukua.”

HABARI MICHEZO

# GUARDIOLA AKATAA KUMLAUMU HAALAND

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amesisitiza kuwa Erling Haaland hakupaswa kulaumiwa kwa Manchester City kupoteza pointi dhidi ya Chelsea licha ya kupiga mashuti tisa bila kufunga bao.


City na Chelsea zilitoka sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Etihad Jumamosi na kuteleza nyuma ya Liverpool na Arsenal - ambazo zote zilishinda mapema siku hiyo, katika mbio za kuwania taji la Ligi Kuu England.

Haaland alipiga mashuti tisa kati ya 31 ya City na akakosa nafasi ya dhahabu katika kipindi cha pili wakati mpira wake wa kichwa kutoka krosi ya Kevin De Bruyne ulipopaa juu ya lango.

Ilikuwa ni idadi kubwa zaidi ya mashuti ambayo Haaland amekuwa nayo bila kufunga katika mchezo wowote akiwa na Man City.

"Ni vizuri kuwa na mashuti tisa na wakati mwingine atafunga," alisema Guardiola.

"Nilikuwa mchezaji wa soka kwa miaka 11 na nilifunga mabao 11. Mimi si mtu sahihi kutoa ushauri kwa washambuliaji.



"Tunatengeneza nafasi, alikuwa na nafasi na wakati mwingine atafunga. Simlaumu. Ni soka, ni binadamu."

Guardiola hakufurahishwa na mchezo wa City kipindi cha kwanza dhidi ya Chelsea, ambao walichukua uongozi muda mfupi kabla ya kipindi cha kwanza cha mapumziko kupitia kwa Raheem Sterling.

Ederson alifanya kazi muhimu ya kuokoa kutoka kwa Sterling katika kipindi cha pili kabla ya Rodri kufunga bao la dakika za lala salama na kudumisha rekodi ya City ya kutoshindwa nyumbani, ambayo ilianzia Novemba 2022.

"Kama timu na kundi, kipindi cha kwanza haikuwa kama tulivyo," alisema Guardiola.

"Mahitaji ni makubwa kwa sababu hakuna mtu atakayetupa, lazima tufanye kila kitu.

"Sisi ni Man City kwa hiyo tunatakiwa kujifanyia kila wakati, kuanzia siku ya kwanza nilisema hivyo inabidi tuboreshe kipindi cha kwanza na kipindi cha pili kilikuwa cha ajabu, kiujumla ilikuwa nzuri sana baada ya kufungwa na Raheem."

## Majeraha ya Jota, Jones pigo Liverpool

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL ilipata majeraha matatu katika ushindi wa mabao 4-1 Jumamosi dhidi ya Brentford, huku Curtis Jones na Diogo Jota wakikabiliwa na majeraha makubwa na mshambuliaji Darwin Nunez akitolewa kwa tatizo "dogo" wakati wa mapumziko.

Ushindi huo ulianzishwa na mkwaju mkali kutoka kwa Nunez katika kipindi cha kwanza, kwa mabao zaidi kutoka kwa Alexis Mac Allister na aliyetokea benchi Mohamed Salah na Cody Gakpo.

Ushindi huo unaimarisha nafasi yao kileleni mwa Ligi Kuu kwa angalau sehemu iliyosalia ya wikiendi.

Hata hivyo, kikosi cha Jurgen Klopp sasa kinapaswa kufanya bila wachezaji muhimu Jones na Jota, huku suala la Nunez likiwa bado halijajulikana.

"Lazima tuone ni kiasi gani inatugharimu - hatujui hilo bado," alisema Klopp katika mkutano na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Curtis aligongwa kwenye sehemu ya chini na ugoko. Tutaona maana yake. Ni kile alichohisi, lakini hakuwa na uhakika wa asilimia 100.

"Diogo anaonekana mbaya zaidi; sikuiona, lakini nilisikia picha hazikuwa nzuri vile vile, kwa hivyo lazima tuone huko."

Klopp alithibitisha kuwa Jones alikuwa akitumia magongo baada ya mechi.

Wanajiunga na orodha ya majeruhi ambayo tayari ilimjumuisha Trent Alexander-Arnold, Thiago Alcantara, Stefan Bajcetic, Ben Doak, Joel Matip, Dominik Szoboszlai na Alisson.

"Hisia zilizochanganyika kwa sababu tulipoteza wachezaji, na hatujui jinsi ilivyo mbaya. Haionekani kuwa nzuri kwa yeyote kati yao (Jones na Jota)," aliongeza Klopp.



## Arteta: Arsenal ipo kwenye kasi ya ubingwa

**LONDON, England**

MIKEL Arteta anaamini kwamba kasi ipo kwa upande wa Arsenal katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu huku wakifikisha mabao 21 katika mechi tano.

Arsenal ilipata ushindi wa mabao 6-0 wikendi iliyopita dhidi ya West Ham na juzi Jumamosi waliwafunga Burnley 5-0.

Martin Odegaard, Bukayo Saka (alifunga mara mbili), Leandro Trossard na Kai Havertz walikuwa wafungaji wa mabao hayo.

"Uhusiano kati ya wachezaji unapita," alisema Arteta, ambaye timu yake imepitwa pointi mbili nyuma ya viongozi, Liverpool.

"Nimefurahishwa sana na utendaji. Mchango wa kila mchezaji mmoja ulikuwa mzuri. Tuna kasi sasa na tunapaswa kuidumisha.



"Kujiamini, ni wakati mzuri. Tunaonesha ufanisi wa hali ya juu mbele ya goli."

Mabao mawili ya Bukayo Saka, yanamaanisha kuwa amefunga mara sita katika michezo yake minne iliyopita - mara ya kwanza katika maisha yake ya soka akifunga katika mechi nne mfululizo.

Akiwa na umri wa miaka 22, Arteta anasema nyota huyo wa England anaonyesha ukomavu zaidi ya miaka yake.

"Tulijaribu kuwafanya wachezaji wetu kutotabirika kwa sababu wapinzani wanatutazama sana na lazima tutafute njia," alisema.

"Bukayo ana uwezo na mazoezi mengi akiwa ndani na karibu na boksi. Leo alikuwa na mabao mawili mazuri sana.

"Tunaona ukomavu huo katika umri wake haswa na wachezaji wa mbele na mawinga. Ni kitu cha ajabu sana kupata, lakini ni ubora alionao."

Odegaard alisherehekea bao lake kwa kuweka mkono wake sikioni kama jibu la ukosoaji wa Jamie Carragher na wengine kwa kupiga picha uwanjani baada ya Arsenal kuishinda Liverpool hivi majuzi.

"Sikuona ishara hiyo, lakini alifurahi sana kwenye chumba cha kubadilishia nguo na jinsi alivyocheza mchezo huo ulikuwa wa kipekee."

HABARI MICHEZO

# LUSAJO ATOA MIFUMO YA MAKOCHA AZAM FC

Na Adam Fungamwango

NAHODHA wa Azam FC, Lusajo Mwaikenda, amefichua mifumo mipya ya makocha wa timu hiyo ambayo inawataka wakati mwingine mabeki wa pembeni kuingia kati na kucheza kama viungo wakabaji.

Lusajo ambaye hucheza beki wa kulia katika kikosi hicho, katika mechi dhidi ya Geita Gold, Ijumaa iliyopita kuna wakati alionekana kuingia ndani na kucheza kama kiungo mkabaji, alisema huo ni mfumo mpya wa makocha wao, Bruno Ferry na Youssoupha Dabo, ambayo inawataka kubadilika kulingana na wakati pamoja na mazingira.

„Ni kweli hiyo ni mifumo ambayo kocha wetu wanatupa, wakati mwingine ‚mafulubeki' tunaombea pembeni, wakati mwingine tunaombea mpira ndani, kuna wakati unaingia ndani kucheza kama kiungo mkabaji, ni nyakati tu ambazo makocha wetu wanataka wakati gani uwe wapi na wewe kama mchezaji inabidi kufuata anachotaka mwalimu," alisema Lusajo ambaye awali alisajiliwa na timu hiyo akiwa kama beki wa kati, kabla ya kubadilishiwa namba na sasa anacheza pembeni.

Lusajo aliendelea kufichua kuwa hata katika mechi dhidi ya Simba walicheza hivyo yeye na mwenzake aliyecheza kushoto, Paschal Msindo kiasi kwamba aliombea mpira akiwa ameingia ndani kutoka kwa Yahaya Zayd na akatoka mbio kwenda pembeni kupiga krosi iliyoipatia bao timu hiyo katika mechi ambayo dakika 90 ziliisha kwa sare ya bao 1-1, Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Alisema mabeki wa Simba hawakumwona kama anaweza kuwa hatari kutokana na sehemu aliyosimama.

„Bado kuna asilimia nyingi hatujaufahamu vizuri mfumo huo sisi wachezaji, ila kama tukiukopi vizuri, tukaukamata mfumo huu sawa sawa na kufika asilimia 90, tutakuwa hatari zaidi kwa wapinzani," alisema.

## Enekia atua Twiga Stars na matumaini

Na Saada Akida

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Twiga Stars, Enekia Kasonga, anayecheza soka la kulipwa katika Klabu ya Eastern Flames ya Saud Arabia, ametua nchini kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi hicho kuelekea mchezo wa kuwania kufuzu Olimpiki dhidi ya Afrika Kusini.

Twiga Stars ina kibarua kigumu cha kutafuta ushindi Ijumaa wiki hii, katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam kabla ya timu hizo kurejeana nchini Afrika Kusini wiki ijayo.

Akizungumza na Nipashe jana, kiungo huyo alisema anafurahi kuwa sehemu ya wachezaji walioitwa kuja kupambania taifa katika mchezo wa kufuzu Olimpiki dhidi ya Afrika Kusini na atapambana kuhakikisha wanafanikiwa kupata ushindi.

Enekia alisema wachezaji waliokuwapo kikosi wanafahamiana na tayari kila mmoja anamjua mwenzake, hivyo kazi kubwa iliyopo ni wao kufuata maelekezo ya benchi la ufundi kimbinu kuhakikisha wanafanikiwa kushinda.

"Benchi la ufundi linaendelea kuandaa mipango ya ushindi kwa kutuandaa vizuri, wachezaji wote hapa tunajuana ninaimani kubwa ya kufanya vizuri katika michezo yote miwili tukianzia nyumbani na kumalizia ugenini," alisema Enekia.

Aliongeza kuwa maandalizi yanaendelea vizuri na kutokana na mbinu za kifundi wanazopewa anaamini watafanya vizuri kwa kupata matokeo chanya katika michezo yote ya kuwania nafasi ya kufuzu Olimpiki.

MBIO ZA NYIKA...




Mkuu wa Uhusiano wa DStv Tanzania, Johnson Mshana, akimvisha medali ya dhahabu mshindi wa kwanza wa mashindano ya taifa ya mbio za nyika Boay Dawi, aliyeibuka mshindi wa kwanza wa mashindano hayo yaliyofanyika hivi karibuni katika viwanja vya Shule ya Sekondari Ilboru, Arusha. Dawi ataungana na wanariadha wenzake 12 wanaounda Timu ya Taifa ya Mbio za Nyika za Dunia zitakazofanyika Machi 30, mwaka huu jijini Belgrade, Serbia. Dawi alitumia muda wa dakika 28:36:80. **MPIGAPICHA**

## Wawa aionya Simba, Benchikha afunguka

INATOKA UK. 24

inzani wao na kwamba kikubwa anahitaji ushindi katika mchezo huo.

Alisema kila eneo analifanyia kazi na kurejea kwa beki wake, Henock Inonga kikosi kimeongeza nguvu kwenye safu ya ulinzi baada ya kukosekana kwenye michezo sita ambayo wameshacheza.

"Asec Mimosas tumekutana nao, tunawafahamu na wao wanatufahamu, tunaandaa mipango yetu ya kwenda kusaka matokeo chanya ugenini, tunaendelea kusahihisha makosa yetu tuliyoyaona katika mechi zilizopita," alisema kocha huyo raia wa Algeria.

Simba chini ya Benchikha inaendelea kujiandaa na mchezo huo na habari nje ni kurejea kwa beki wao, Inonga ambaye alikuwa na timu yake ya Taifa, DR Congo iliyofanikiwa kumaliza nafasi ya nne katika michuano ya AFCON.

## MUDATHIR AANIKA SIRI MABAO YANGA

INATOKA UK. 24

yote uwanjani, kukaba, kuchezesha na kushambulia kwa kufika ndani ya boksi, nitafunga sana, nimeambiwa nifanye yote kwa sababu ya uwezo wangu wa kucheza nafasi nyingi uwanjani," alisema Mudathir.

Aliongeza kuwa hataki kumuangusha kocha wake kwa sababu amemwamini na kumpa nafasi hali ambayo inamfanya kujitoa na kupambana kuhakikisha anaisaidia timu yake kuvuna pointi tatu katika michezo ya hiyo ya ligi kuu na wiki hii wakielekea mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mudathir alisema anatarajia kuendelea kufunga katika michezo ya ligi hiyo kuhakikisha wanatetea taji lao la ubingwa na michezo ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa kwa kutafuta pointi tatu dhidi ya CR Belouizdad watakaocheza Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na Machi Mosi, mwaka huu nchini Misri dhidi ya Al Ahly.

Kiungo huyo amefikisha mabao sita huku akijiweka rekodi ya kuwa mkali wa kutibua mipango na kusaidia timu yake kupa pointi katika michezo migumu na muhimu.

Michezo

Jumatatu Februari 19, 2024

Nipashe

Rashford atajwa PSG kumrithi Mbappe UKURASA 21



# WAWA AIONYA SIMBA SC, BENCHIKHA AFUNGUKA

●●●Ni kuelekea mechi dhidi ya Asec Mimosas, ataja maeneo ya kuchungwa, asema...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, akipigia hesabu pointi tatu dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, aliyekuwa beki wa Wekundu wa Msimbazi hao Pascal Wawa, amewaonya mabeki wa timu yake hiyo ya zamani kuwa makini na safu ya ushambuliaji ya wapinzani wao.

Ijumaa wiki hii Simba itashuka dimbani nchini Ivory Coast kucheza mechi yao ya raundi ya tano dhidi ya Asec Mimosas ikiwania nafasi ya kufuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Wawa raia wa Ivory Coast aliyezichezea Simba, Singida Fountain Gate FC na sasa yupo nchini kwao, amewang'ata sikio Wekundu wa Msimbazi akiwataka mabeki wa timu hiyo kuwa makini na safu ya ushambuliaji ya wapinzani kwani ni hatari, kutokana na kucheza pasi fupi fupi za kuwachanganya na kuwachosha wapinzani, wanapokuwa na mpira kuelekea kufanya mashambulizi.

Alisema mara chache hubadilika kulingana na kasi ya mpinzani, hivyo Simba wanatakiwa kuwa makini hasa safu ya ulinzi kuhakikisha hawatoi nafasi ya kushambuliwa hasa kipindi cha kwanza kuruhusu bao.

"Nawafahamu Simba vizuri hasa inapokuwa kwenye mechi za kimataifa, wako vizuri, ninaamini wakiwa makini safu ya ulinzi na washambuliaji wakitumia nafasi zinazopatikana, nina matumaini makubwa watapata ushindi hapa Ivory Coast," alisema Wawa.

Katika hatua nyingine kocha Benchikha alisema anaendelea kukisuka kikosi chake kulingana na aina ya mpira anaocheza mp-




Benchikha

INAENDELEA UK. 23

# Mudathir aanika siri mabao Yanga



Mudathir

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuwasha moto mkali katika kufumania nyavu, kiungo mkabaji wa Yanga, Mudathir Yahya, amesema siri kubwa ya kufunga mabao msimu huu ni baada ya Kocha Mkuu wa timu hiyo, Miguel Gamondi, kumwongezea majukumu ndani ya uwanja.

Kwa mara nyingine tena, juzi Mudathir alifunga mabao mawili dhidi ya KMC, Yanga ikishinda 3-0, huo ukiwa ni mwendelezo wa kufunga mfululizo baada ya mechi zilizopita kufunga Yanga 1-0 dhidi ya Namungo, Yanga 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji FC na wakati wakiichapa 2-1 dhidi Mashujaa FC.

Akizungumza na Nipashe jana, Mudathir, alisema kulingana na majukumu hayo anaamini ataendelea kufunga sana kwa sababu anatakiwa kukaba, kuchezesha na kazi kubwa kuhakikisha ashambulia kwa kufika katika boksi la mpinzani.

Alisema mabao sita aliyofunga ni kwa aina moja, baada ya kufuata maelekezo aliyopewa na Gamondi, kumtaka uwanjani kufanya majukumu yake na zaidi kupanda kushambulia kwa kufika ndani ya 18 ya mpinzani wanapokuwa na mpira.

Alisema jukumu la kuzuia pale wapinzani wanapokuwa na mpira anatakiwa kuhakikisha hawafiki katika eneo lao na kusababisha madhara jambo ambalo amekuwa analifanya sana msimu huu chini ya Gamondi.

"Tangu nimeanza soka 2013, msimu huu nafunga sana, hakuna siri yoyote zaidi kujitoa na kujituma na kufanyia kazi mipango ya kocha ambaya anataka nijiongeze kwenye boksi, na ninafanya hivyo na kufunga.

"Gamondi ananipa majukumu

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >